

**Moshi** mweusi penzi la Harmonize, Kajala

UKURASA 20




**Mane** ndio mchezaji bora wa Afrika – Rashford

UKURASA 21

**MAISHA**

Nipashe Jumapili — Baba, Mama na Mwana



Anaongea kingereza, lakini mbumbumbu



MAISHA NI NYUMBA
Hizi ndizo kero za madalali kwa watu wanaotaka kupanga



HARUSI



MAKALIO MAKUBWA
Urembo unaopendwa, lakini hatari

UKURASA 9


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Aprili 4, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580540

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Waziri atoa hofu wafanyabiashara

• **Ataka** waache kuficha fedha, asema hakuna atakayechota zikiwa benki... *Endelea ukurasa 2*



Rais, Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, akitokea jijini Dodoma. **PICHA: IKULU**

## Kishindo cha Rais Samia siku 15 tu chashtua

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

## Njia muhimu za kufuata kuepuka kujifungua mtoto mwenye ulemavu

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


**MICHEZO** NAMUNGO FC, NKANA MAJARIBUNI LEO UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kishindo cha Samia siku 15 usipime

**Na Gwamaka Alipipi**

KISHINDO kikuu. Ndivyo inavyoweza kuelezwa juu ya mambo aliyoyafanya Rais Samia Suluhu Hassan baada ya jana kutimiza siku 15 madarakani tangu alipoapishwa kushika wadhifa huo Machi 19, mwaka huu.

Samia alichukua nafasi hiyo kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Tangu ashike usukukani, Rais Samia ametawala vichwa vya habari kwa uamuzi anaouchukua juu ya mambo mbalimbali, ikiwamo msimamo wake, mabadiliko ya hapo kwa hapo na hotuba zake zenye mvuto.

Katika kipindi hicho, Rais Samia ameshafanya mabadiliko magumu ya kiuongozi kwa kumbadilisha Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Bashiru Ally, na kumteua Balozi Hussein Katanga kuchukua nafasi hiyo. Uamuzi huo umewafanya Watanzania wabaki wakijiuliza maswali pasipo kuwa na majibu.

Sambamba na hilo Machi 28, mwaka huu Rais Samia alitangaza kumsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko, ikiwa muda mfupi baada ya kupokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na ile ya utendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Katika hotuba hiyo, Rais Samia ndipo alipoonyesha yale aliyosema wakati wa mazishi ya kitaifa ya Hayati Dk. Magufuli, Dodoma kuwa wale wenye wasiwasi naye kama ataweza kushika mikoba ya mtangulizi wake, sasa anaweza.

Rais Samia tangu aingine madarakani amekuwa kiongozi mwenye msimamo. hilo alilidhihirisha akiwa jijini Dodoma wakati wa hotuba yake ya mazishi ya kitaifa ya kifo cha Hayati John Magufuli. Akihutubia maelfu ya wananchi waliojitokeza na viongozi ya kimataifa katika Uwanja wa Jamhuri, Rais Samia aliwahakikishia Watanzania kuwa wanaomwangalia kwa wasiwasi watamtambua kadri muda unavyosonga.

Aliweka wazi kwamba aliyesimama mbele yao ndiye Rais wa Tanzania mwenye maumbile ya mwanamke. Hata wakati anaapishwa kushika urais, alisema hakuna kitakachoharibika chini ya uongozi wake.

Katika hafla ya kupokea ripoti ya CAG, alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo, kuimulika TPA haraka kutokana na ubadhirifu uliopo na kutangaza kumsimamisha Kakoko ili kupisha uchunguzi.

Machi 31, Rais Samia wakati wa kuapishwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, jijini Dodoma, aliwashangaza tena Watanzania na wageni waalikwa waliohudhuria shughuli hiyo kwa kufanya 'surprise' ya kutangaza mabadiliko ya baraza la mawaziri. Katika mabadiliko aliyotangaza, Rais Samia aliwahamisha baadhi ya mawaziri kutoka wizara moja kwenda nyingine, huku wengine wakisalia kwenye wizara zao.

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliinyooshea kidole Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliyokuwa ikiongozwa na Waziri Selemani Jafo, kuwa kuna upotevu mkubwa wa fedha katika wizara hiyo na kumtaka waziri huyo kusimamia mapato na matumizi ya wizara hiyo na akishindwa aseme ili asaidiwe.

Ndani ya siku 15 Rais Samia pia amegusia kuhusiana na suala la rushwa ya ngono katika vyuo vikuu nchini na kusema kuwa utafiti wa aina hiyo ya rushwa katika vyuo uangaliwe kwa kina badala yake TAKUKURU ijikite katika suala la uvujishaji mitihani.

**FARAJA WALIPAKODI**

Aprili Mosi, Rais Samia wakati wa hafla ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua aliibua faraja kwa wafanyabiashara huku akionya utaratibu wa kudai kodi kwa nguvu kuwa unachangia kufunga biashara, hivyo kupunguza mapato ya serikali.

Aliweka wazi kwamba utaratibu unaotumika sasa katika kudai kodi kwa wafanyabiashara una ukakasi, akikemea kudai kodi kwa nguvu, kushikilia akaunti za benki za wafanyabiashara na kuchota fedha.





Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza katika kikao kazi cha wizara hiyo cha kushughulikia maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan na kero zinazowakabili walipa kodi nchini, jijini Dodoma, jana. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# Waziri atoa hofu wafanyabiashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewataka wafanyabiashara waache kuficha fedha nyumbani na badala yake wapeleke benki huku akiwatoa hofu kwamba hakuna mtu atakayezichukua.

Mwigulu alisema hayo wakati wa kikao kazi alichokiitisha kwa ajili ya kuchakata maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na kuanza kushughulikia kero za kodi zinazowakabili walipakodi nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri Mwigulu alisema katika kikao hicho amekutana na idara za Wizara pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ili kuchakata maelekezo hayo na kutengeneza mazingira ya ukusanyaji kodi yasiyoua biashara za walipakodi.

"Kwa wale wafanyabiashara ambao walishaanza kuona nikiweka hela yangu benki ikaonekana mtandaoni labda itachukuliwa yote, nitoe wito kuwa warudishe fedha kwenye mabenki (benki), zitaliwa huku na mchwa na panya bila sababu.

Uchumi wa kisasa si wa kuweka fedha kwenye boksi, kodi itatozwa tu sehemu ya fedha itakayotakiwa kukusanywa," alisema.

Katika kikao hicho cha jana, alisema jambo la msingi walililoliangalia ni maelekezo yaliyotolewa na Rais hivi karibuni katika matukio makubwa ya kitaifa, siku ya kupokea ripoti ya CAG na TAKUKURU na hotuba ya uapisho wa Makamu wa Rais na mawaziri, "alisema.

Alisema katika hotuba za Rais kuna majukumu ambayo Wizara ya Fedha na Mipango imepewa maelekezo yenye nia njema kwa nchi.

"Ili tuendelee na kupata mapato makubwa kwa nchi yetu lazima tukuze uchumi ndipo tutapata mapato. sasa Rais ameliangalia na kulipa uzito unaostahili kwamba tukuze uchumi ndipo tutapata wigo mpana wa kukusanya mapato yetu.

"Sisi Wizara na taasisi zinazohusika, hili jambo lazima tulifanyie kazi na tulitekeleze ipasavyo. Kila mtu kwenye idara yake hili jambo ajipange nalo tukuze uchumi na tutengeneze walipa kodi, tuwalinde na walipa kodi waliopo tusiwaue," alisema.

Waziri huyo alisema sheria na taratibu zipo na wataalam walirekebishe pale ambapo wameenda kinyume cha sheria na weledi.

"Turudi kwenye mstari tulinde uchumi wetu na tusiue walipa kodi kwa kuua shughuli zao, tunapoua vyanzo vya mapato yetu, tunaua walipa kodi wetu, tuna mambo mengi yamekuwa yakihusianishwa na athari hiyo ya kuharibu uwezekano wa kuongezeka kwa walipa kodi au kukua kwa shughuli za kuongeza mapato hayo tuyaache," alisema.

Alitaja mambo ambayo yanajitokeza kwenye mijadala mbalimbali bungeni ni namna wanavyokadiria kodi.

"Ukadiriaji wa kodi zetu, tuufanye kwa kuzingatia sheria na weledi. Ukusanyaji wa mapato kuna maeneo ambayo yamekuwa yakijitokeza na kuleta mkanganyiko tuyaache.

"Kwa mfano anatokea mtu amekadiriwa miaka yote kodi na amepewa cheti, inapita miaka 10 anaenda kukadiriwa tena anapigia tena na miaka mingine ya nyuma ambayo miaka yote alishapewa cheti... utaratibu unaotumika unahusisha ofisi na mhusika na kila mwaka anakuwa 'cleared' halafu anakwenda kuendelea na shughuli zake anaambiwa alete taarifa za nyuma, hiyo tuiache," alisema.

Alisisitiza ukadiriaji huo ufuate sheria na taratibu bila kumwonea mfanyabiashara.

Akizungumzia suala la kushika akaunti na fedha za walipa kodi, Waziri Mwigulu alisisitiza TRA wazingatie maelekezo ya Rais na wazingatie weledi katika kukusanya kodi.

"Sisi Wizara tutaendelea kuyafuatilia haya. Kuna wale ambao mara zote huwa wanabadili maelekezo, nitoe angalizo mapema, ulipotolewa msisitizo tukusanye kodi wale wengine walikuwa wanakwenda na kuvamia tumeambiwa tukusanye kodi hadi mtakoma, sasa hivi wameambiwa kusanyeni kwa weledi wataenda kusema sasa hivi ni kula kuku tu.

"Nchi hii tutajenga wenyewe kwa kodi kinachotakiwa ni kuzingatia weledi katika kukusanya kodi, tutashindwaje na wazee wetu wa vijijini, akiwa na ng'ombe wake hawezi kukamua ng'ombe mjamzito, na wanakamua na kumuachia mtoto, na hawakamui hadi damu, hawa hawajaenda shule yeyote lakini ukitafsiri maelekezo ya Rais tukusanye kwa weledi tusiue biashara ya yule tunayemtoza,"alisema.

"Tutoze kodi tusichukue fedha za watu, kodi ni sehemu ya fedha kisheria unayopaswa kukusanya, tusichungulie kuona mtu ana fedha kiasi gani tunachukua zote, tukusanye kiwango kinachotakiwa kutozwa, tusichukue fedha za watu tunazoziona," aliongeza.

Alitoa rai kwa Watanzania kuzingatia sheria ili kuepuka kujiweka kwenye mazingira yatakayosababisha usumbufu.

"Utoaji kodi ni kipimo cha juu cha uzalendo, Watanzania huu utamaduni wa kulipa kodi liwe jambo la kawaida kwenye maisha yetu, janja janja ya kukwepa kodi hiyo ni kuvunja sheria na halitavumilika,"alisema.

Kadhalika, alisema serikali itaangalia mifumo bora ya kukusanya kodi ili kulinda mapato ya serikali.

"Mkakati wa serikali ni kupunguza mlipano wa mkono kwa mkono, tuzingatie taratibu zinazotolewa, tunapokwenda mbele zaidi tutaangalia mifumo bora ya makusanyo inayotumika ili kulinda mapato ya serikali, na hii tutazingatia ili wananchi walipe kodi kwa hiari bila shuruti na haipotei inafika kwenye mfuko wa serikali,"alisema.

HABARI KITAIFA

# Siku zahesabika mrithi wa Bashiru CCM

**Na Waandishi Wetu**

LEO kunatarajiwa kuwa na mabadiliko mengine ya uongozi ndani ya serikali, Rais Samia Suluhu Hassan, akitarajiwa kuapisha makatibu wakuu wapya wa wizara 23 zilizopo.

Mabadiliko hayo aliyadokeza mwenyewe siku tatu zilizopita alipowaapisha viongozi aliowateua Jumatano, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Wakati hali ikiwa hivyo serikalini, ndani na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kunaendelea mchakato wa kupata Katibu Mkuu mpya wa chama hicho atakayerithi mikoba ya Dk. Bashiru Ally.

Februari 26, mwaka huu, aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, alimteua Dk. Bashiru kuwa Katibu Mkuu Kiongozi akirithi nafasi ya Balozi John Kijazi aliyefariki dunia na kuapishwa Februari 27. Siku iliyokuwa ya mwisho kwa Hayati Rais Magufuli kuonekana hadharani katika shughuli za kitaifa.

Kutokana na uteuzi huo wa Dk. Bashiru ambaye Jumatano aliteuliwa na Rais Samia kuwa mbunge, akimpisha Balozi Hussein Katanga kwenye nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi, kulimaanisha kwamba kiti cha Katibu Mkuu wa CCM kiko wazi.

Katiba ya CCM inabainisha kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa ndiye mwenye mamlaka ya kupendekeza jina la Katibu Mkuu wa chama hicho. Hata hivyo, kiti cha Mwenyekiti wa CCM nacho kiko wazi kutokana na kufariki dunia kwa Rais Magufuli.

Kwa kulitambua hilo, tayari uongozi wa juu wa chama hicho ulioketi Machi 30, mwaka huu, kupitisha jina la mgombea mbunge wa Muhambwe mkoani Kigoma na kuridhia mapendekezo ya Rais Samia ya jina la Makamu wa Rais, ulipanga tarehe ya kumpata Mwenyekiti wa CCM Taifa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma siku hiyo na Katibu wa NEC - Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, mkutano mkuu maalum wa kufanya uamuzi huo umepangwa kufanyika Aprili 30, mwaka huu, yaani siku 26 zijazo.

Ni katika mkutano huo maalum mrithi wa Dk. Bashiru anatarajiwa kupendekezwa na Mwenyekiti mpya wa CCM na kupitishwa na wajumbe husika.

**MSEKWA ATIA NENO**

Aliyekuwa Spika wa Bunge, Pius Msekwa (pichani), ametaja sifa zinazombeba kiongozi kuwa Katibu Mkuu wa CCM, akigusia uwezekano wa Dk. Bashiru kurejeshwa kwenye nafasi hiyo.



Spika Msekwa, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, alisema sifa mojawapo ni kuwa mwanachama wa CCM na anayekifahamu kwa undani chama hicho.

"Nilishawahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM, sifa ya kwanza ni lazima uwe mwanachama wa CCM, mtu yeyote hawezi kuwa Katibu Mkuu kama siyo mwanachama wa CCM," alisema.

Spika Msekwa aliongezea: "Baada ya hapo sifa za huyo kama inafanyika uteuzi mpya, basi sifa za huyo atakayeteuliwa zitaangaliwa na mwenye mamlaka ya kuteua, maana yake kila mteuliwa anateuliwa na mamlaka fulani."

Alisema kwa hali inavyokuwa ndani ya CCM na anavyofahamu, Mwenyekiti wa CCM Taifa ndiye anateua kwa maana ya kupendekeza jina la Katibu Mkuu wa chama kwa kikao kinachomchagua na kwa kawaida atapendekeza jina na kukubaliwa kwa sababu Katibu Mkuu ndiye mtendaji mkuu msaidizi wa Mwenyekiti wa Taifa.

"Jibu sahihi ni kwamba ukiondoa sifa ya msingi ya uanachama, sifa ya yule atakayeteuliwa wakati huo inategemea anavyoonekana na mwenye mamlaka ya kuteua, kwa sababu wana CCM wapo wengi, huwezi kusema lazima awe msomi, wasomi wapo wengi, mengine hayajahitaji kuorodheshwa kwa sasa kwa sababu katika dunia ya sasa shirika lolote lile linaendeshwa kwa digitali kwa maandishi.

"Kwa hiyo, mtu lazima awe msomi, hii nayo siyo lazima kutajwa, ukishataja ya msingi zilizobaki anaangalia yule mwenye kuteua kwa sababu wanakuwa ni wengi wenye sifa za kufanana, yeye mwenye kuteua anataka mtu wa namna gani."

Alipoulizwa uwezekano wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru kurudisha kwenye nafasi hiyo, Spika Msekwa alisema jambo hilo linawezekana ingawa linategemea na mwenye mamlaka ya kuteua. "Mimi nilisharudishwa mara mbili, nilikuwa Katibu Mkuu Mtendaji wa tano, nikapelekwa kwenye kazi nyingine, baadaye nikarudishwa nikawa Katibu Mtendaji," alisema.

Spika Msekwa alisema kurudishwa kwa mtu katika nafasi yake ya zamani siyo jambo la ajabu kwa kuwa limeshamtokea katika uongozi wake.

"Hili linaweza kutokea kwa yoyote yule kuteuliwa mara mbili kushika nafasi hiyo moja, hakuna kuzuizi cha kufanya hivyo, inategemea matakwa ya mamlaka ya uteuzi katika kumrejesha Bashiru," alihitimisha.

● **Imeandikwa na Beatrice Shayo na Sanula Athanas.**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED

TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Mdhibiti wa Sekta ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta nchini. Pamoja na mambo mengine, ina jukumu la kusimamia gharama na tozo katika huduma za mawasiliano zinazotolewa na Watoa huduma na kuwalinda watumiaji wa huduma hizo.

Mnamo tarehe 5 Februari, 2021, TCRA ilitoa tangazo la kukaribisha maoni ya wadau kuhusu huduma za vifurushi zinazotolewa na Watoa huduma za mawasiliano ya simu za mikononi.

Kutokana na maoni hayo, TCRA iliandaa Kanuni ndogo za Vifurushi (Rules) za mwaka 2021, zenye lengo la kuweka utaratibu kwa Watoa huduma wa namna ya kupanga vifurushi, bei na muda wa matumizi ya vifurushi hivyo. Kanuni hizo zimeanza kutumika tarehe 02 Aprili, 2021.

Katika utekelezaji wa Kanuni hizi, watoa huduma waliwasilisha idadi na bei ya vifurushi vipya pamoja na bei za huduma nje ya vifurushi. TCRA imeidhinisha idadi ya vifurushi vilivyowasilishwa pamoja na bei za huduma nje ya vifurushi na tayari zimeanza kutumika tarehe 02 Aprili 2021.

Hata hivyo, TCRA imesitisha kwa muda matumizi ya bei mpya ya vifurushi vya data ili kutoa nafasi kwa Watoa huduma kupanga upya bei za vifurushi kwa ufanisi na kufanya uchambuzi wa kina kwa ajili ya kulinda maslahi ya watumiaji.

TCRA itaendelea kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu huduma za mawasiliano kwa ustawi na maendeleo ya Taifa.

IMETOLEWA NA MKURUGENZI MKUU
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
Tarehe 02 Aprili, 2021

Na Romana Mallya

# Fanya haya usijifungue mtoto mwenye ulemavu

KILA mwanamke mwenye uwezo wa kubeba ujauzito anapoupata huwa na matarajio baada ya miezi tisa kujifungua salama na kupata mtoto asiye na matatizo na dosari zozote za kiafya na maumbile.

Lakini, ni ukweli usiopingika kwamba siyo wanawake wote wanaobeba ujauzito hujifungua watoto timilifu. Wapo ambao hujifungua wenye ulemavu.

Ikumbukwe kuwa zipo dosari za kimaumbile ambazo hutokana na kurithi, mfano zitokanazo na wazazi kuwa na kansa.

Kupitia makala hii, Daktari Bingwa wa Wazazi na Magonjwa ya Kike kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Athanael Mtinangi, anaeleza sababu za kitaalamu zinazochangia mtoto kuzaliwa akiwa na ulemavu.

Katika mahojiano maalum na Nipashe, Dk. Mtinangi anataja sababu mbalimbali zikiwamo mama kuwa na uzito mkubwa, kurithi, kutumia dawa za miti shamba, msongo wa mawazo na kutotumia dawa za folic acid.

Dk. Mtinangi anasema wajawazito wenye uzito mkubwa au unene kupita kiasi, wako hatarini kujifungua watoto wenye ulemavu.

Hii inadhibitishwa pia na utafiti uliofanywa na watafiti wa kisayansi wa Chuo Kikuu cha Stockholm cha Sweden, ulioonyesha tatizo la kuzaa watoto walemavu hutokea iwapo mama anakuwa mnene kabla ya kutungwa kwa mimba ambapo kwa mujibu wa utafiti huo, watoto zaidi 43,550 wanazaliwa wakiwa walemavu kutokana na mama zao kuwa wanene kila mwaka.

Dk. Mtinangi, akielezea zaidi kuhusu suala la unene uliopitiliza, anasema kundi hilo huzaa watoto wenye uzito mkubwa ambao hupita kwenye njia ndogo.

"Hii ndiyo tunaita uzazi pingamizi, kipindi mtoto anazaliwa anakuwa anapita kwenye njia ndogo, hivyo kichwa chake kinakuwa kinabanwa na anapotoka pia hatalia mapema na kitendo cha kutokulia mapema kinasababisha hewa isifike haraka kwenye ubongo.

"Wanawake wanene huzaa watoto wenye uzito mkubwa kuanzia kilo nne na zaidi na hii husababishwa na kwanza wao ni wanene na wana hifadhi kubwa ya sukari kwenye miili yao, na sukari huleta madhara mengi ikiwa ni pamoja na kuingiza vitu ambavyo mwili hauvihitaji," anafafanua.

Dk. Mtinangi anawataka wajawazito wahudhurie kliniki mapema iwezekanavyo pindi wanapogundua wana ujauzito, ili vitu kama hivyo vibainike mapema na kama atakuwa na mtoto mkubwa baada ya kufanyiwa vipimo, atafanyiwa upasuaji badala ya kujifungua kawaida.

"Sababu za uzazi pingamizi zinafahamika na zitajulikana kliniki kama mtoto ni mkubwa au nyonga ya mama ni ndogo au mama anakuwa na ulemavu wa nyonga au wengine unaweza kukuta kwa sababu mimba za kwanza na hajawahi kujifungua, anapokwenda kujifungua saikolojia yake inamfanya akazaa mtoto mwenye shida na akaishia kwenye ulemavu wa akili," anafafanua.



Wajawazito wanatakiwa kuhudhuria kliniki mapema iwezekanavyo pindi wanapogundua wana ujauzito.
PICHA: MAKTABA

Anawashauri wanawake wakiwamo wenye uzito mkubwa kupitiliza pindi wanapobaini ni wajawazito, wanatakiwa kwenda kliniki ili kama kuna tatizo ligundulike mapema.

"Unene pia ni kitu ambacho kinatoka kwenye familia, kuna familia fulani watu wanazaliwa wanene, huwezi kuwakataza wasizaliwe wanene au wasizae watoto wanene.

"Wanapokuja kliniki huwa tunamfuatilia, tutaangalia nyonga kama ipo sawa na mtoto akifika wiki ya 38 huwa tunampima kwa kumfanyia Ultra Sound kuangalia uzito wa mtoto na kumshauri," anasema.

Dk. Mtinangi anasema kama mtoto hatazaliwa kwa wakati unaotakiwa au kutokupata huduma stahiki baada ya kuzaliwa, atapata tatizo la kukosa hewa kwenye ubongo.

"Kwa hiyo, ubongo ukikosa hewa tu kidogo mara nyingi watoto kujikuta wanazaliwa na ulemavu wa akili kwa sababu baada ya kuzaliwa ubongo wake haukupata hewa haraka, mtoto anapokuwa tumboni humtegemea mama yake," anasema.

Dk. Mtinangi anataja ulemavu mwingine ni wa mtoto kuumia wakati anazaliwa ambao hutokana na utaalamu wa mzalishaji.

"Unakuta wakati akimzalisha mama, akamvunja mtoto mkono, bega au akamvunja miguu au eneo lingine na hii huwa inatibika haraka.

"Unakuta mtoto wakati anazaliwa kwa kutanguliza miguu akavunjia mguu au mkono au bega yanatibiwa haraka, sanasana kinachokuja kutokea ni ulemavu wa akili," anasema.

Anafafanua zaidi kuhusu mtoto kutopata hewa ya kutosha kwenye ubongo, akisema anapokuwa tumboni, hutegemea damu ya mama yake na kwamba huwa hapumui.

"Wakati mtoto akiwa tumboni huwa hapumui, lakini anapozaliwa tu katika kipindi cha dakika moja, lazima alie ili aanze kujitegemea mwenyewe, kama hatapewa msaada wakati alipotoka tu na yeye alikuwa hajitegemei, alikuwa anategemea, asipopewa msaada na mtu wa karibu, anaweza kushindwa kuhema kwa dakika moja.

"Hii dakika moja huwa inatakiwa mtoto apanue mdomo alie ili hewa iingie kwenye mapafu iende kwenye moyo na ikishatoka kwenye moyo iende kwenye maeneo mengine ya mwili ambapo eneo muhimu la kwanza ni ubongo ambapo ubongo utapeleka taarifa maeneo mengine yafanye kazi vizuri," anafafanua.

Mtalaamu huyo anasema kuboreshwa kwa huduma za afya kumewezesha kupunguza matatizo mbalimbali, yakiwamo ya watoto kuzaliwa wakiwa na ulemavu.

"Katika kina mama tisa wanaojifungua, asilimia 90 hujifungua watoto ambao hawana shida sana, asilimia tisa katika hiyo asilimia 90 ndiyo huitaji msaada, huu ni utafiti wakati tunafanya mafunzo ya kuwafundisha watu kuwezesha kuwasaidia watoto wanapozaliwa, hizi zilikuwa wakati ule ila kwa sasa huduma zimeboreshwa karibu hospitali nyingi," anasifu.

Anasema walikuwa wanafundisha kwa sababu walijua kuwa asilimia tisa ya watoto wanaozaliwa, watahitaji msaada wa kufutwa na kuangaliwa shida zao na asilimia moja huhitaji kuhamishiwa hospitali za rufani ili kupata huduma kubwa zaidi na mara nyingine huwapoteza.

"Huu ni utafiti wa kutoa msaada siyo takwimu, kwenye takwimu lazima uingie kwenye vitabu uangalie watoto wangapi wamezaliwa kwa mwezi na wangapi hawakupata hewa," anasena.

Kuhusu matumizi ya dawa ya Folic Acid, anasema wataalamu wamekuwa wakihimiza wajawazito wazitumie hususani kutatua matatizo ya kidonda cha mgongoni, mdomo sungura na ulemavu mwingine.

"Folic Acid inapatikana kwenye vyakula kama mtu atakula mlo kamili, lakini siyo kila mtu anaweza kupata mlo kamili unaotakiwa wakati wote wa ujauzito au kawaida, ndiyo maana tunasisitiza matumizi ya dawa hizi, Folic Acid ni moja ya vitu muhimu hutumika kumuumba mtoto na mahitaji ya uendeshaji wa mwili kwa ujumla," anabainisha

Hata hivyo, anasema wapo watoto wanaozaliwa wenye ulemavu unaotokana na kurithi kwenye ukoo.

**UTAFITI WA STOCKHOLM**

Mmoja wa watafiti wake, Dk. Martina Persson, anakaririwa kwenye chapisho la kitabibu 'Medical Journal'kuwa hatari ya watoto kuzaliwa wakiwa walemavu imeongezeka kwa asilimia 4.7 huku wengi wao wakizaliwa na ulemavu wa miguu, macho, mikono na matatizo ya moyo.

Akielezea uhusiano uliopo baina ya unene na kuzaliwa kwa watoto walemavu, Dk. Raul Artal anasema wanawake wengi ambao ni wanene kupitiliza, wana magonjwa kama kisukari na shiniko la damu hivyo husababisha watoto kutokamilika baadhi ya viungo kutokana na presha ya mwili wa mama mjamzito.

## HABARI KITAIFA



Samwel Nyungu ambaye ni mjukuu wa mnufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF), Yared Nyungu (hayupo pichani), wa Kijiji cha Solowu, wilayani Chamwino mkoani Dodoma, akiwaonyesha waandishi wa habari na viongozi wa mpango huo juzi, mashine ya kufua vyuma iliyotengenezwa na babu yake baada ya kuwezeshwa fedha na TASAF. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# UWT yawapa neno wateule wa Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), umewataka viongozi waliopata nafasi ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuwatumikia wananchi kwa weledi na kulinda viapo vyao ikiwamo kujiepusha na ubadhirifu wa mali za umma.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudentia Kabaka, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akitoa salamu za pole kwa kifo cha Hayati Rais John Magufuli na pongezi kwa Rais Samia kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke Tanzania.

"Tumpongeze mama huyu kwanza ni mwanachama wetu wa UWT hai, kwa hiyo tunajipongeza kwa kumtoa Rais katika nchi yetu na tumeona baada ya kuwa Rais ameanza kuteua kuweka safu yake ya uongozi, tumeona Watanzania wakimpongeza na kukubaliana naye na kusema uteuzi wa Dk. Philip Mpango ni chaguo sahihi, kwa hiyo ameanza vizuri,"alisema.

Kabaka alisema UWT inajivunia kuona mwanachama wake amekuwa kiongozi wa juu na kuahidi kumpa ushirikiano wa hali ya juu kwake na kwa serikali yake.

"Nimeangalia katika Afrika Mashariki, Tanzania ni nchi ya pili kuwa na Makamu wa Rais mwanamke, wa kwanza alikuwa Uganda, lakini kwa Mama Samia amekuwa Rais kamili kwa Katiba yetu na kwa Afrika ni Rais wa tatu," alisema.

Alimpongeza Rais Samia kwa nafasi hiyo kwa kuwa anazosifa licha ya taratibu za kikatiba.

"Mama Samia anasifa za kuwa Rais, na alimsaidia sana Hayati Magufuli kwa umahiri mkubwa na sasa Tanzania ni salama chini ya uongozi wake, ana uzoefu wa kutosha," alisema.

Alimshukuru na kumpongeza kwa kuwaamini wanawake katika Baraza lake la Mawaziri ambapo amewateua na kuongeza idadi ya wanawake Mawaziri.

"Tunachofurahi zaidi katika zile Wizara ambazo sisi tunafikiri zinagusa wananchi zaidi ndio zimepewa wanawake, kwa mfano Wizara ya Afya, Elimu, Mambo ya Nje, TAMISEMI, tunafikiri ameona wanawake wanaweza na tunaamini watamsaidia kazi, kwa kuwa hizi ndio Wizara zinatuletea ushindi kwa CCM, hizi zinagusa wananchi moja kwa moja," alisema na kuwasihi Watanzania kumpatia ushirikiano Rais ili afanye kazi kwa ufanisi.

"Viongozi aliowaamini chapeni kazi, wanawake tuchape kazi kwa umahiri zaidi na kuishi kwenye viapo vyetu, tusiwe wabadhirifu wa mali za umma na tuwatumikie wananchi bila ubaguzi," alisema.

# Ummy ataja vipaumbele 6 TAMISEMI

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ametaja vipaumbele sita atakavyoanza navyo, huku akibainisha kwamba ofisi hiyo si ngumu kuiongoza kama watu wanavyodhani.

Miongoni mwa vipaumbele alivyovitaja Waziri Ummy ni kuimarisha usimamizi wa makusanyo ya ndani na matumizi katika mamlaka za serikali za mitaa.

Kipaumbele kingine ni kupitia hoja zilizoibuliwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hususani halmashauri nane zilizopata hati chafu na 53 zilizopata hati ya mashaka.

Pia amegusia ushirikiano na ubunifu, usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo na urejeshaji wa fedha za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Waziri Ummy akizungumza juzi na menejimenti ya ofisi hiyo jijini hapa, alisema bado kuna mianya mingi ya upotevu wa mapato ya halmashauri na kipaumbele chake ni kudhibiti na kusimamia mapato yanayopatikana.

"Kipaumbele changu cha kwanza ni kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri ili zijitegemee na kutatua changamoto za wananchi zilizopo katika sekta ya afya, elimu na miundombinu," alisema.

Alisema Aprili 6, mwaka huu, atatoa maelekezo kwa sekretarieti za mikoa na wakurugenzi wa halmashauri baada ya kupitia hoja za CAG. "Kuna watu wanasema TAMISEMI ni ngumu, mimi nasema TAMISEMI si ngumu. Kama ni ngumu maana yake mmeshindwa kunisaidia mimi na naibu mawaziri kutekeleza wajibu wetu. Tunakubali ni kubwa lakini hakuna kigumu kama tutafanya kazi kwa umoja, uratibu na ufanisi kati yetu na katibu mkuu kiongozi amesisitiza hilo," alisema.

Waziri huyo alisema mtangulizi wake, Selemani Jafo, alifanya kazi kubwa na nzuri na kwamba wakati anaingia mapato yalikuwa asilimia 60 kwa sasa yamefikia asilimia 94.

"Kuna kazi imefanyika na binafsi nataka kuwapongeza wote kwa kile ambacho kimefanyika. Lakini sote tunakubaliana kwamba bado kuna kazi kubwa ya kufanya na mimi pamoja na naibu mawaziri. Kipaumbele chetu ni kimoja tu kuimarisha ukusanyaji wa mapato na matumizi," alisema Waziri Ummy.

Aidha, aliagiza kufanyika mapitio ya haraka kwenye hati za mashaka kwenye halmashauri 53.

"Mmemsikia Spika (Job Ndugai) hivi mkurugenzi unakuwaje na amani wakati watoto wanakaa chini, hivi sisi TAMISEMI tunashindwa kuja na mkakati wa kuondoa tatizo la watoto kukaa chini? Hivi TAMISEMI tunashindwa kuhakikisha madarasa yanajengwa ili watoto wasirundikane kwenye madarasa au kuwa na madawati na madarasa? Nyumba za walimu hiki ni kipaumbele changu," alisema.

Kuhusu utoaji wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Waziri Ummy alitaka kujua fedha zilizorejeshwa na kuzitaka halmashauri kueleza urejeshaji wake.

# Samia apongezwa kwa kuanza vizuri

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Hazina iliyoko Magomeni jijini Dar es Salaam imempongeza Rais Samia Suluhu kwa kuapishwa kuwa Rais na kupongeza kasi nzuri aliyoanza nayo.

Akzungumza na gazeti hili, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Omari Juma, alisema wadau wa elimu wana imani kubwa na Rais Samia kwamba ataendelea kusimamia na kukuza sekta ya elimu hapa nchini.

Juma alisema kwa uzoefu alionao, Rais Samia ataiongoa nchi kwa weledi mkubwa na kwa kushirikisha sekta binafsi anaamini sekta ya elimu itakwenda mbali zaidi.

"Sisi wadau wa elimu tunampongeza na tunaahidi kumpa ushirikiano mkubwa katika kazi zake kama rais na tunawaomba wadau wengine wampe ushirikiano ili aweze kutekeleza majukumu yake," alisema.

Alisema Rais Samia amekuwa serikalini kwa muda mrefu, hivyo uzoefu wake umewafanya Watanzania wawe na matumaini makubwa kwamba atawavusha kwenye maendeleo ya kweli katika sekta mbalimbali.

"Shule ya Hazina imekuwa ikifanya vizuri kwenye matokeo ya Kata, Wilaya, Mkoa na Kitaifa hivyo kwenye taaluma sisi tunaahidi kwamba tutaendelea kufundisha na kutoa elimu bora kama ambavyo tumekuwa tukifanya kama mchango wetu wa kukuza sekta ya elimu nchini," alisema.

Alitoa mfano kuwa mwishoni mwa mwaka jana wanafunzi wa shule hiyo walitia fora kwa kuongoza kwenye usaili wa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule maarufu nchini. Alisema wanafunzi wengi wa shule hiyo waliokwenda kufanya usaili kwenye shule zenye majina makubwa walifanikiwa kuongoza na kupata nafasi za kujiunga kidato cha kwanza.

Alitoa mfano kuwa mwanafunzi aliyeongoza kwenye usaili kwenye shule maarufu ya Feza Boys alitoka Hazina na kwamba wanafunzi wa shule hiyo wamekuwa wakiongoza kila mwaka kwenye usaili.

Alisema kwenye usaili wa mwaka jana wanafunzi sita wa Hazina walifanikiwa kufanya vizuri zaidi kwenye usaili na kujiunga na shule za Marian zilizoko Bagamoyo Mkoa wa Pwani.

Wanafunzi sita wa Hazina, alisema walifanya kufanya vizuri zaidi na kujiunga na shule za Feza wakati wanafunzi wengine tisa walifanya vizuri na kujiunga na shule ya wavulana ya Shamsiye.

"Mwaka 2019 tulipeleka wanafunzi wengi sana kwenye shule hizo na waliongoza na wazazi wengi wanapenda sana watoto wakimaliza shule ya msingi wakasome shule nzuri ndiyo sababu wanapenda kuwaleta hapa Hazina," alisema

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha vifurushi, gharama za simu kipatiwe ufumbuzi

**TANGU** kuingia kwa mitandao ya simu za mkononi nchini, kumekuwa na unafuu wa huduma kulinganisha na ilivyokuwa kabla ya ujio huo. Yote hiyo ni kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yamesababisha madhara kuwa rahisi zaidi.

Kutokana na maendeleo hayo, mtu anaweza kutumia simu kwa ajili ya kupiga na kuzungumza mambo binafsi, kibiashara na hata ya kikazi. Sambamba na hayo mtu anaweza kutumia mtandao wa simu kwa ajili ya kutuma na kupokea fedha, kutuma ujumbe mfupi wa maneno au sauti na kufanya mawasiliano kwa njia ya intaneti.

Sambamba na hayo, matumizi ya simu pia yamepanua wigo wa mawasiliano kwa kuwa hivi sasa zinatumika hata kuwasiliana kupitia mitandao ya kijamii kama vile facebook, twitter na instagram. Kadhalika matumizi hayo ya simu yametoa wigo mpana zaidi wa elimu kwa kuwa watu wanajifunza mambo mbalimbali kulingana na mahitaji yao.

Hali hiyo ni tofauti na zamani watu walipokuwa wakitumia simu za mezani ambazo watu wachache ndio waliokuwa wanazimiliki, watu kusoma baruapepe na taarifa mbalimbali ama ofisini au kwenye ofisi zilizokuwa na kompyuta na zimeunganishwa na intaneti.

Pamoja na kuwapo kwa unafuu wa upashanaji wa habari kupitia simu za mkononi, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa watumiaji kuwa wamekuwa hawatendewi haki na kampuni zinazotoa huduma hiyo ya mawasiliano hasa katika gharama za kupiga simu na vifurushi vya mitandao.


Kwa mujibu wa watumiaji wa mitandao hiyo, kampuni za simu zimekuwa zikitoa vivutio mbalimbali vya vifurushi lakini matumizi yanakuwa tofauti. Mtu ananunua kifurushi cha wiki, kwa mfano, anaweza kutumia kwa siku mbili tu na kuambiwa kimekwisha!

Jambo hilo limesababisha malalamiko makubwa kutoka kwa watumiaji na hatimaye serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ikaiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kushughulikia tatizo hilo. Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya habari, Dk. Faustine Ndugulile, bila kuuma maneno, aliitaka TCRA kufanyia kazi malalamiko hayo ambayo alisema wateja wamekosa imani na kampuni za simu.

Licha ya kutekeleza agizo hilo lililotolewa Desemba 29, mwaka jana, kampuni hizo juzi zilitangaza kuwa zimefanya mabadiliko ambayo wananchi walipokea kwa mtazamo hasi kwamba hakuna unafuu wowote.

Ghadhabu zilizoonyeshwa na wananchi kupitia ujumbe waliotoa kupitia mitandao ya kijamii, ni ishara kwamba wamekosa imani na kinachofanywa na kampuni za simu. Upande wa pili, serikali pia kupitia mdhibiti wa sekta hiyo, TCRA, pia inapokea lawama kutokana na kutokuchukua hatua dhidi ya watoa huduma.

Ni vyema sasa suala hili likafikia tamati kwa kampuni za simu kutenda haki kwa wateja kupitia vifurushi zinavyotangaza lakini kiuhalisia vinawaumiza watumiaji. TCRA pia ihakikishe kuwa wananchi wanapata haki katika matumizi ya simu kulingana na kile wanacholipa.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii iendelee kujihadhari, kupambana na kifua kikuu

**MACHI** 24 ya kila mwaka, huwa ni maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu na Ukoma Duniani. Tanzania huungana na nchi zingine duniani kuadhimisha siku hiyo.

Mwaka huu, Tanzania haikufanya maadhimisho hayo kutokana na msiba mkubwa ulioli kumba taifa kwa kuondokewa na Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli aliyefariki dunia Machi 17.

Pamoja na hayo, kifua kikuu kinatajwa kuwa miongoni mwa magonjwa ambayo yanawakumba watu wengi maskini na kwamba wanaoathirika kwa kiasi kikubwa, ni wale wanaotoka katika nchi zinazoendelea.

Pia inaelezwa na wataalam wa afya kuwa kuna aina kuu tatu za kifua kikuu, kikiwamo ambacho hutokea pale ambapo bakteria waliopo mwilini wapo hai na kinga ya mwili imeshindwa kuwadhibiti wasisababishe madhara. Watu wenye tatizo hilo, wanaweza kuambukiza wengine kwa njia ya kuvuta pumzi kama watakohoa, kutema mate, kupiga chafya, kupiga kelele, ikiwa watafanya vitendo hivyo karibu na watu wasio na ugonjwa huo.

Aina nyingine ya ugonjwa inatajwa kuwa ni ile isiyo na madhara, kitaalam ikiitwa latent TB. Mtu mwenye latent TB, hana dalili za ugonjwa huo, hajisikii kuwa mgonjwa na hawezi kuambukiza mtu mwingine kifua kikuu. Lakini pia, aina hiyo inaweza kujirudia na kuathiri sehemu ya juu ya mapafu na kusababisha kikohozi cha kawaida ambacho baadaye huongezeka na kusababisha mtu kukohoa damu.

Aidha, mtu anaweza kuwa na homa, kupungukiwa hamu ya kula, kupungua uzito bila sababu ya msingi na wakati mwingine, anaweza kutokwa na jasho kwa wingi kuliko kawaida wakati wa usiku.

Aina ya tatu ya kifua kikuu inatajwa kuwa ni ugonjwa uliosambaa mwilini, na kwamba hiyo hutokea pale ambapo kinga ya mwili imepungua na kusababisha ugonjwa huo kuenea kupitia damu hadi sehemu nyingine za mwili.

Sehemu hizo za mwili ni mifupa, mishipa ya fahamu, ngozi, figo, kibofu cha mkojo, ngozi ya moyo (pericadium), mfumo wa uzazi, viunganishi vya mifupa (joints) na lymphatic system, ambapo husababisha homa, kupungua hamu ya kula, kuchoka na kupungua uzito.

Pamoja na kwamba inawezekana huo ni ugonjwa wa kudumu katika nchi zinazoendelea, kifua kikuu kinaweza kuzuilika iwapo kila mmoja wetu atafuata na kuzingatia maelekezo ya watalaam wa afya.

Ninaeleza hivyo kwa sababu zaidi ya watu 4,000 wanakufa kwa kifua kikuu kila siku duniani, huku wengine karibu milioni 10 wakiambukizwa ugonjwa huo kila mwaka duniani.

Katika maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani mwaka jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus, alitoa taarifa kuwa unaathiri mapafu na kusababisha mtu kuwa hatarini. Wakati idadi hiyo ikitajwa kuambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu, anafafanua kuwa wanajitokeza watu wachache kwa ajili ya kupata dawa muhimu za kuokoa maisha yao.

Lakini habari njema ni kwamba, wakati kukiwa na taarifa hiyo, Tanzania inazidi kuendelea kupiga hatua katika kupunguza kasi ya maambukizo mapya ya ugonjwa wa kifua kikuu kwa asilimia 18 kwa mwaka 2020.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika kilele cha kupokea taarifa ya tathmini ya mpango mkakati wa tano wa mwaka (2015-2020) wa Kifua Kikuu na Ukoma inaeleza hayo. Hadi kufikia mwaka jana, wizara iliongeza uwezo wa ugunduzi na kuibua wagonjwa wengi zaidi kutoka asilimia 29 mwaka 2015 hadi asilimia 53 mwaka jana, na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi saba duniani zilizofikia malengo hayo ya mwaka 2020 ya kupunguza maambukizo mapya.

Hiyo inatokana na kwamba mwaka jana tu wizara imefanikiwa kugundua wagonjwa karibu 82140, na kwamba kadri inavyogundua wagonjwa wengi, ndivyo inavyojitahidi kuzuia maambukizo zaidi.

Kwa kuwa inaelezwa kuwa ugonjwa huo ni hatari, lakini pia kinazuilika, umefika sasa kwa kila mmoja wetu kutafakari na kuchukua hatua za kukabiliana na nao ili kuwa salama zaidi.

Wataalam wa afya wanapotoa ushauri huo wa jinsi ya kujikinga na kifua kikuu, kinachobaki na sisi wenyewe kuuzingatia, ili kuepuka kuambukiza au kuambukizwa kifua kikuu.

SAFU

AFYA

# Siri katika bilinganya kwa afya

Na Mwandishi Wetu



BILINGANYA ni aina ya tunda ambalo limekuwa likitumiwa na watu kwa namna mbalimbali kwa ajili ya chakula.

Wengi wanaitumia kama mboga kwa kuchanganya na mbonga zingine ili kuongeza ladha au kuitumia yenyewe kama mboga kwa kuichemsha ikiwa chukuchuku au kuunga na viungo kaka nyanya na vitunguu.

Nchini India ambako watu wake ni magwiji katika ulaji wa mazao jamii ya matunda na viungo kama pilipili na bamia, bilinganya imepewa nafasi ya juu na imekuwa ikiitwa 'mfalme wa mboga'.

Pamoja na kwamba ni chakula ambacho hulinda mwili dhidi ya magonjwa, baadhi ya watu hupuuza kuitumia. Wakati mwingine, baadhi ya watu huona ni kama chakula cha watu wa hali duni ambao hawawezi kumudu gharama za maisha. Kumbe kwa kufanya hivyo, wanashindwa kuelewa kuwa ni mlinzi wa afya zao.

Wataalamu wa afya wanasema bilinganya ni kiboko katika kupambana na kuzuia magonjwa na hatari mbalimbali mwilini. Miongoni mwa manufaa ya kutumia tunda hilo, kwa namna iwayo yote katika mwili ni;-

**Vidonda vya tumbo**

Watu wengi duniani wanasumbuliwa na vidonda vya tumbo, hivyo kulazimika kutumia dawa mbalimbali. Kwa wenye tatizo la vidonda vya tumbo, inaelezwa kuwa wanapotumia tunda hilo kama mboga, wana uwezekano mkubwa wa kupona.

Kama ilivyoelezwa awali, bilinganya inaweza kupikwa kama ilivyo na kuliwa ama na ugali au wali. Lakini pia inaweza kuchanganywa kwenye nyama yoyote na kuongeza ladha na utamu katika chakula.

**Tiba ya jipu**

Baadhi ya watu wamekuwa wakisumbuliwa na majipu ama kutokana na mchafuko wa damu mwilini au mabadiliko ya hali ya hewa hasa wakati wa joto. Kwa wenye tatizo hilo, hii ni habari njema kwamba bilinganya ni mwarobaini wa majipu.

Kwa mtu anayesumbuliwa na tatizo hilo au mtoto wake amepata jipu, anashauriwa kupondaponda likiwa bichi kisha paka sehemu yenye tatizo.

**Tiba ya Usingizi**



Una tatizo la kukosa usingizi? Jibu la tatizo limepatikana. Mtu mwenye tatizo hilo anashauriwa kula bilinganya na tatizo lake litapungua kwa kiasi kikubwa au kumalizika kabisa.

Mtu mwenye tatizo kama hilo, anatakiwa kula biringanya mara kwa mara na ataona matokeo yake baada ya muda mfupi.

**Kiboko ya sumu**

Kutokana na matumizi mbalimbali ya vyakula na vinywaji vyenye kemikali, watu wamekuwa wakipata tatizo la sumu mwilini. Matokeo yake husababisha madhara mbalimbali hata kupoteza maisha.

Ili kupunguza tatizo hilo na kuongeza muda wa kuishi, inaelezwa kuwa tunda hili lina uwezo wa kuondoa sumu mbalimbali mwilini, hivyo ni muhimu watu wakalitumia kwa faida hiyo.

**Kupunguza uzito, kisukari**

Mtindo wa maisha ya sasa hasa ulaji wa vyakula bila mpangilio hasa vile vyenye mafuta mengi, umesababisha watu wengi kuwa na uzito uliopilitiza. Matokeo yake, watu wengi hukumbwa na shinikizo la damu na hata kisukari na hata kupoteza maisha.

Ili kuepuka matatizo kama hayo au kwa wale waliokwisha kukumbwa nayo kupata ahueni, inashauriwa watumie tunda hilo na wataona matokeo yake ndani ya muda mfupi tangu kuanza.

Aidha, kwa wale ambao wanasumbuliwa na maradhi ya kisukari, ambayo pia husababishwa na mtindo wa maisha, kwa maana ulaji wa vyakula bila mpangilio, wanashauriwa kutumia bilinganya kwa kuwa husaidia kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa huo.

Zaidi, kwa wale wenye matatizo ya ukuaji wa nywele, inaelezwa kuwa utumiaji wa juisi ya tunda hilo husaidia kukuza nywele.

Pia ni msaada katika ulinzi wa ngozi ya mwili. Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, bilinganya hufanya ngozi kuwa na mwonekano mzuri na yenye afya bora.

Sambamba na hilo, inaelezwa kuwa bilinganya ni kinga dhidi ya matatizo kwenye ubongo.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Acheni tucharazwe ni haki yetu



Na Joseph Kulangwa

Wabongo wakala mkong'oto kama vitoto vya shule na kilio juu. Xiao Yong na mwenzake, nasikia ndio walikuwa wamekamata bakora wakiwashikisha adabu Wabongo hao kama vichekechea vilivyojikojolea.

FIKIRIA umemtembelea jamaa yako nyumbani kwake, ukiwa sebuleni mara anatokea paka anaelekea vilipo vyombo vya chakula, anavinusanusa. Bila shaka utashtuka na kumkemea 'wee' au 'eishtoka' au 'acha!'

Pamoja na kumkemea, paka huyo anakutazama kwa dharau na kuendelea kunusa, kana kwamba hakusikia lolote. Utamshangaa ni paka gani huyu asiyeogopa, lakini pengine utajisemea moyoni, kazoea watu au kazoezwa, utajikalia kimya.

Mara anatokea mwenyeji wako, anamwona na kumtishia kumpiga teke au kibao, paka huyo atatoka baruti na kutokomea nje. Bila shaka utaelewa kuwa kumbe hakuzoea kukemewa akaacha, bali kupigwa.

Hata baadhi ya binadamu wako kama huyo paka. Bila kipigo hawaendi na hususan watoto. Watu wazima kichapo kwa kweli si stahiki yao wala staha, na kwa kweli hata heshima tu ya kibinadamu.

Hivyo, inapotokea ukaona au kusikia binadamu kampiga binadamu mwenzake, na hasa si kumpiga tu bali kumcharaza viboko kama mwanafunzi au mtoto, basi ujue mpigaji alikemea akashindwa, akaona mwenyeji anapiga ndipo naye akaiga.

Hivi karibuni mkoani Mbeya katika kampuni inaitwa Bonanza, kuna taarifa zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii, zikidai kuwa raia wa kichina walicharaza wafanyakazi wao Watanzania, baada ya kufanya makosa katika kampuni hiyo ya michezo ya kubahatisha.

Wabongo wakala mkong'oto kama vitoto vya shule na kilio juu. Xiao Yong na mwenzake, nasikia ndio walikuwa wamekamata bakora wakiwashikisha adabu Wabongo hao kama vichekechea vilivyojikojolea.

Nilipoiona klipu ile nikajiuliza, hivi Wabongo tunakosea wapi? Hivi kweli Wachina waje nchini kwetu kutucharaza kama ilivyokuwa enzi za wakoloni Waarabu na Wajerumani kweli? Hebu waende Kanda Maalumu pale juu wafanye hivi waone!

Lakini ukitafakari sana utaona ni sawa tu, wacha watucharaze tu, kwani wanatofauti gani na yule Mkuu wa Mkoa aliyeondoka ofisini kwake, akavamia shule na kuwapora walimu madaraka na kucharaza viboko wanafunzi? Kisa wamefanya fujo shule kusababisha hasara!

Wachina hao wanatofautianaje na Mkuu wa Wilaya kule Arusha aliyechomoka ofisini kwake na kwenda shuleni kushuhudia madawati yaliyoibwa na kukusanya wachomelea vyuma wenye sharubu zao na kuwacharaza viboko hadharani?

Eti, hao kina NhuwahuwanChingching, wana tofauti gani na yule Naibu Waziri aliyechoropoka wizarani na kwenda Kinondoni kusaka ombaomba na kuwacharaza viboko hadharani wasaidizi wa ombaomba hao?

Hakuna tofauti yoyote kati ya wakubwa hawa na hao Chingching, wote hawakufuata sheria, wote walishika mikwaju na kucharaza watu makalioni, wote walifanya hivyo hadharani tena mchana kweupe watu wakishuhudia. Sasa wanatofauti gani?

Tofauti ni kuwa ya Mbeya hayakufika Polisi kumlalamikia Arasii, ya Arusha polisi hawakujihusisha dhidi ya Disii hata ya Kinondoni hatukuona gwanda lolote likimsaka Naibu, sasa iweje kwa Wachingching ambao waliiga kutoka kwa wakuu wetu hawa?

Haina tofauti na ya yule mgeni na paka mnusa vyombo, kwamba alifokewa akaendelea kunusa, lakini alipotishiwa kupigwa teke au kibao, huyo akawahi akatoroka. Kwa hiyo mgeni akajifunza, kwamba kumbe nikija siku nyingine nikamwona nyau akinusa, ni teke au magumi tu.

Kama ndivyo, Chingching akimlamba bakora Mbongo baada ya kuona mfano kwa viongozi tena wateule, kwanini asiamini kuwa ndio utaratibu unaotumika katika nchi hii, kwamba ukikosa ni viboko pale pale sehemu ile ile uliyopo, hakuna Polisi wala Mahakama!

Walisema Wahenga, ukienda kwa mwenye chongo nawe vunja lako jicho ili ufananefanane nao, vinginevyo utatengwa na kuonekana ama unawadharau au unawabagua na kitakachokupata usilalamike. Viboko hadharani woyeee!

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# TAWA katika hili mnaifedhehesha serikali



Na Thobias Mwanakatwe

**Mmoja wa wananchi waliohudhuria mkutano huo anasimama na kusoma maazimio waliyoyafikia na wananchi katika kikao chao kuwa hawakubaliani na upimaji ardhi wenye lengo la kuvimega vijiji vyao.**

NI Machi 31, saa 12:00 asubuhi naianza safari kutoka Mwenge, Dar es Salaam kwenda Vikumbulu Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani.

Ni mwendo wa takribani saa tatu hadi kufika katika kata hiyo. Kabla ya kufika unapitia vijiji vya Kitonga Chole, Mtunani, Panga la Mwingereza, Chole, Kurui, Yombo Lukinga, Msanga na Boga.

Vingine ni Mengwa, Kikwete, Mfuru, Chang'ombe, Masanganya, Kibuta, Kauzeni, Masaki, Sungwi, Kisanga, Kazimzumbwi. Vigama, Kisarawe, Pugu hatimaye unafika kijiji cha Vikumbulu.

Kinachonipeleka huko kama mwanahabari ni kusikiliza wananchi kuhusu kilio cha mgogoro wa mpaka ambao umetokana na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuanza kumega maeneo ya ardhi ya vijiji hivyo na kuviingiza kwenye hifadhi bila kuwashirikisha.

Baada ya kufika tu, wenyeji wangu wananipokea kwa furaha na katika hili nabaini kuwa furaha yao hiyo ina mambo mawili. Mosi, wanaona ujio wangu kilio chao kitasikika mbali na pili, wananieleza kuwa ni mara chache sana kutembelewa na wanahabari ili kutoa kero zinazowasibu.

Baada ya takribani saa moja kunaitishwa mkutano wa viongozi wa serikali za vijiji vitatu ambavyo ni Mtunani, Kitonga Chole na Panga la Mwingereza vinavyopakana na hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, zamani ikiitwa Selous.

Mkutano huo lengo kubwa la kuitishwa ni kuweka msimamo kuhusu upimaji ardhi unaoendelea katika vijiji hivyo ili kuvimega na kuviingiza ndani ya hifadhi, unaendeshwa na Diwani wa Kata ya Vikumburu, Siri Gongo, na viongozi wengine wa kata.

Mmoja wa wananchi waliohudhuria mkutano huo anasimama na kusoma maazimio waliyoyafikia na wananchi katika kikao chao kuwa hawakubaliani na upimaji ardhi wenye lengo la kuvimega vijiji vyao.

Mwananchi huyo anasema upimaji mpya wa ardhi katika vijiji vyao unakiuka sheria, kanuni na taratibu kwa kuwa haujazingatia mipaka ya asili kati ya hifadhi na vijiji husika na pia unafanywa katika maeneo yaliyopimwa na kupangiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Hata hivyo, kinachonishtua kwenye mkutano huo ni baada ya kujitokeza mwananchi mmoja, Mbwana Telenga, akilia kwa uchungu akisema alipigwa risasi na askari wa TAWA.

Anasema alipigwa risasi katika mguu wake wa kushoto na kuvunjwa mfupa Agosti 9 mwaka jana kwa kile alichoeleza kuwa aliingia ndani ya hifadhi wakati akiokota kuni.

Anaongeza kuwa anachokumbuka hakuwa ndani ya hifadhi kama ilivyoelezwa na askari hao isipokuwa ni mgogoro wa muda mrefu kati ya wananchi na askari wa TAWA na TANAPA ambao hawana uhusiano mzuri na wananchi.

Anasema baada ya kupigwa risasi alipelekwa na askari hao katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) ambako matibabu yake hadi anapona, anadaiwa Sh. 434,497 deni ambalo hadi sasa hajalipa kwa sababu limetelekezwa na TAWA.

Mwananchi huyo ambaye sasa anatembelea magongo, anasema kutokana na hali yake ilivyo, alitakiwa awe anakwenda kufanyiwa vipimo mara kwa mara lakini anashindwa kwenda hospitalini sababu anadaiwa na hana uwezo wa kulipa fedha hizo.

Anamalizia kwa kusema katika hali ya kushangaza askari waliofanya tukio hilo hawajachukuliwa hatua zozote na wanaendelea na kazi kama kawaida wakila maisha licha ya tukio hilo kuripotiwa katika kituo cha polisi Kisarawe.

Binafsi, naliona tukio hili kama TAWA wanaifedhehesha serikali na kufanya wananchi waichukie serikali yao pendwa.

Kitendo cha kumpiga mwananchi risasi halafu mnamwachia deni la matibabu apambane nalo si jambo zuri hata kama pengine huyo mwananchi alikuwa na kosa au la.

Viongozi wetu katika Wizara ya Maliasili na Utalii wamekuwa wakisisitiza na kuwaomba wananchi wawe rafiki na walinzi hifadhi zetu lakini ninachokiona kwa TAWA hawataki kujenga mahusiano na wananchi.

TAWA hao hao Februari, 2019 walikamata wakulima wanane wa vijiji hivyo vitatu na kufunguliwa kesi namba 55/2019 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro kwa madai kuwa walikuwa wakilima ndani ya hifadhi.

Wakulima hao walipokamatwa walinyang'anywa vifaa mbalimbali vikiwamo matrekta, jembe na mbegu ambavyo katika hali ya kushangaza, vilirejeshwa na kukabidhiwa kwa wakulima Februari 11, mwaka huu, ikiwa ni miaka miwili tangu vilipokamatwa baada ya wananchi kuhangaika kila ofisi ya serikali.

Kimsingi huu ni unyanyasaji ambao hauwezi kuvumiliwa, TAWA inabidi wabadilike katika utendaji wao na kuwa rafiki kwa wananchi hususani walio karibu na hifadhi.

Kitu cha kushangaza viongozi wa TAWA ambao walifika kijijini hapo, siku ya mkutano hawakutaka kushiriki mkutano huo wa wananchi badala yake walikaa pembeni.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.**

## DARASA LA NDOA

# Mambo ya kuzingatia wakati wa uchumba - 1



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Uchumba si ndoa, bali ni hatua ya msingi na daraja la kuingia katika ndoa. Hivyo, uchumba unaweza kuvunjika muda wowote. Wako baadhi ya watu waliosomesha, kuwanunulia vitu vya thamani wachumba ikiwa ni pamoja na gari, nyumba, kiwanja na samani.**

UCHUMBA huanza na urafiki. Mtu anaweza kuwa na marafiki wengi, lakini mchumba huwa ni mmoja tu, ambaye hutokana na marafiki alio nao.

Uamuzi wa kuoa au kuolewa ni muhimu zaidi na mzito kuliko wa kununua nyumba au gari. Ni uamuzi muhimu sana ambao mtu anafanya kuhusu maisha yake, hivyo utulivu, umakini na mwongozo ya Mungu vinahitajika ili kumwezesha mtu kufanya uamuzi makini.

Ni muhimu ikazingatiwa kuwa, kinachotokea kabla ya ndoa, kuna uwezekano mkubwa kuendelea kutokea wakati wa ndoa. Mchumba akiwa na hasira wakati wa uchumba, ni dhahiri katika ndoa anaweza kuwa na hasira zaidi. Mchumba akiwa mwongo au akiwa na tamaa, si mwaminifu, basi baada ya ndoa anaweza kuwa balaa zaidi.

Pamoja na kuwa mapenzi ni upofu, ni muhimu kuchukua tahadhari pale viashiria vibaya vinapojitokeza wakati wa uchumba. Usilewe mapenzi na kulazimisha uchumba kama huna hakika na mchumba wako.

Waswahili wanasema, heri nusu shari kuliko shari kamili. Ukioa au kuolewa na mtu asiye sahihi, baada ya ndoa utavuna maumivu. Makosa yakifanyika katika uchumba, yanaathiri ndoa. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya uamuzi makini katika uchumba. Mfahamu vizuri unayemchumbia, kwani waswahili wanasema, "si vyote ving'aavyo ni dhahabu."

Uchumba si ndoa, bali ni hatua ya msingi na daraja la kuingia katika ndoa. Hivyo, uchumba unaweza kuvunjika muda wowote. Wako baadhi ya watu waliosomesha, kuwanunulia vitu vya thamani wachumba ikiwa ni pamoja na gari, nyumba, kiwanja na samani. Uhusiano upovunjika wengi wao wamejikuta katika majuto na maumivu makubwa kiasi cha kutishia kutaka kujiua.

Kwa mantiki hii, haishauriwi wachumba kuwekeza pamoja wakati wa uchumba. Wakati mzuri na unaofaa kuwekeza pamoja ni baada ya ndoa kufungwa au kuoana.

Vijana wengi wamejikuta katika matatizo mengi baada ya kuoa au kuolewa kwa sababu ya kukosa umakini. Wengi wao wameingia katika uhusiano wa kukurupuka bila kuzingatia mambo ya msingi hivyo kujikuta katika maumivu.

Ili kuhakikisha kuna baraka na maisha yasiyo na matatizo katika ndia, kuna mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa ucuhumba. Miongoni mwa mambo hayo ni kama yafuatayo;-

**Kusudi la maisha**

Usifurahie na kuvutiwa na sherehe za ndoa za wengine, bali jiulize kwa nini unataka kuoa au kuolewa? Umejipanga kuwa mume/mke wa mtu? Unajitambua kuwa wewe ni mtu wa aina gani?

Pia lazima kujiuliza una hakika kuwa unazo sifa za kuwa mke/mume wa mtu? Si kila mtu ana sifa ya kuwa mume au mke wa mtu. Fahamu kuwa kutokuwa na kusudi na mpango katika maisha ni kuchagua kushindwa maisha ya ndoa.

**Muda wa kutosha kumfahamu mtu**

Chunguza, fahamu, na jiridhishe kuhusu mila na desturi za kabila lake. Fahamu familia anayotoka na misingi ya imani yake katika Mungu; pima upendo wake kama niwa bandia.

Upendo wa kweli hauvutwi na mali, fedha, vitu au mwonekano pekee kama umbo au sura kwani mwonekano wa mtu wa nje haumaanishi kuwa ndio ubora wake. Mvuto wa nje, cheo au nafasi ya kazi na elimu visiwe kigezo pekee cha kumchagua mtu. Jiongeze!

Fahamu haiba na tabia zake. Angalia mtu asiyejirahisisha kwako. Kujirahisisha ni kiashiria cha kukosa ubora na sifa za kuwa mke/mume wa mtu.

Zingatia kwamba ili upate mtu bora, wewe mwenyewe uwe bora kwanza. Mara nyingi mtu hutafuta mtu wa namna yake.

**Mshirikishe Mungu**

Kupata mwenzi anayefaa ni mtihani mzito. Inahitaji muda na maandalizi. Usitumainie akili zako tu. Mshirikishe Mungu pia. Huwezi kupata mwenzi anayefaa Mungu asipohusika. Mwenzi mwema hutoka kwa Mungu. Mungu atakuelekeza na kusema nawe, ukimtumaini yeye.

**Epuka mashinikizo**

Kuoa au kuolewa ni jambo la hiari. Usioe/kuolewa kwa mashinikizo, hivyo uamuzi makini unahitajika. Uamuzi wa siku moja unaweza kujenga au kubomoa maisha yako yote.

**Zingatia muda**

Tambua wakati mwafaka wa kufanya uamuzi wa ndiyo au hapana kwa kuwa hata katika hatua ya uchumba kuna nafasi ya kufanya uamuzi thabiti. Muda wa uchumba ni muda wa kupokea majibu ya Mungu kwamba ndiyo au hapana.

Tambua pia tabia hatarishi mapema. Tabia hatarishi ni kiashiria kuwa mtu huyo si sahihi kwako, hivyo uhusiano usilazimishwe. Waswahili wanasema: "Heri ya nusu shari kuliko shari kamili."

**Itaendelea Jumapili Ijayo**

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255 744000066.]**

# MAISHA

APRILI 4, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 10

## Anaongea kingereza, lakini mbumbumbu



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Hizi ndizo kero za madalali kwa watu wanaotaka kupanga



## HARUSI

Ukurasa 12



### MAKALIO MAKUBWA

# Urembo unaopendwa, lakini hatari

Ukurasa 14

# Anaongea Kingereza, lakini mbumbumbu

**Na Moses Ismail**

NI kweli, Kiingeleza anachoongea ni fasaha kabisa. Ni kile kile cha kutoka kwa Malikia, hababahatishi katika lugha hiyo, anaijua kikweli kweli.

Msingi wa kuijua lugha hiyo ni shule anayosoma, anasoma 'intaneshino skuli', ambayo msingi wa elimu yao ni ule wa Uingereza na lugha rasmi ya masomo shuleni kwao ni Kiingereza.



Kwa sababu hiyo anakijua hasa Kiingereza na anawashangaza watu wengi wa mtaani pale wanapomuona 'katoto kadogo' kanavyoongea 'Kiinglishi'.

Na kwa sababu ya kuongea lugha hiyo kwa ufasaha, wazazi wake pamoja na watu wengine mtaani wanamuona kama 'msomi' sana. Vipi asionekane msomi wakati anaitafuna lugha hiyo iliyokuja na majahazi kama anawazimu?

Hebu jaribu kumwambia akutajie majina ya vitu na viumbe vinavyozunguuka mazingira yetu, atakutajia majina yote, hadi jina la sisimizi, kwa lugha hiyo ya Malikia tena bila kufikiria hata kwa nukta moja.

Geuza sasa maswali yako na muulize maswali mengine juu ya masomo yake na masuala mengine ya kawaida tu ya ufahamu wa jumla ambao unategemea mtoto wa umri na darasa lake awe anatafahamu. Utazimia kwa majibu yake!

Sio wote, ila wengi wa watoto wanaosoma shule hizi ni 'watupu' katika uelewa wa mambo ya 'masomo'. Ukiacha kiingeleza chao wanachokiongea kwa ufasaha, hawana lolote kwenye ufahamu wa masomo na taaluma.

Linaweza kuwa ni suala lenye mjadala mpana na upinzani pia, toka kwa watetezi wa elimu ya aina hiyo, lakini lipime hili kwa kuangalia matoke ya kila mara ya mitihani ya ngazi mbalimbali za elimu ya shule za msingi hadi sekondari.

Utashangaa namna wanafunzi wa shule za mitaala hiyo wanavyofanya vibaya kwenye taaluma na kuangushwa na shule za 'Saint Kayumba' ambao Kiingeleza chao kinatia kichefuchefu kukisikiliza. Bado wanafanya vizuri kitaaluma.

Lakini 'kitaani', uswahilini, ukaanzisha mjadala wa ipi inatoa elimu bora kati ya shule za mifumo hii miwili, 'English medium school' na'Saint Kayumba', utagundua kwa nini wazazi wenye uwezo hupeleka watoto shule za 'kiinglish'.

Wanachozingatia wengi ni ule ufahamu wa haraka wa lugha ya Kiingereza wanaoupata watoto katika shule hizo ambao hufanya waonekana wasomi. Hawajali suala la ufahamu wa taaluma. Watakuuliza, taaluma inasaidia nini?

Lakini je, kujua lugha ya kigeni inaweza kuwa ndio kipimo cha ubora wa elimu?

Kama jibu ni ndiyo, mbona mtaani kuna vijana wengi wanajua Kigiriki, Kitaliano, Kifaransa na hata Kichina? Hawa pia ni wasomi kwa sababu wanafahamu lugha hizo? Hatufikiri kuwa tunahitaji mjadala mpana juu ya suala hili?ends

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

## QUIZ

**Andika kitenzi Ouvrir (yaani kufungua) katika nyakati tofauti kama zilivyoainishwa hapo chini.**

**Indicatif**
**présent**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous……………
vous ……………
ils/elles ……………

**imparfait**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………

**future simple**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………

**passé simple**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………

**passé compose**
j' ai ……………
tu as ……………
il/elle a ……………
nousavons ……………
vousavez ……………
ils/ellesont ……………

**plus – que – parfait**
j' ………ouvert
tu ………ouvert
il/elle ………ouvert
nous………ouvert
vous………ouvert
ils/elles………ouvert

**futurantérieur**
j' ………ouvert
tu ………ouvert
il/elle ………ouvert
nous ………ouvert
vous ………ouvert
ils/elles ………ouvert

**passéantérieur**
j' eus
……………
tueus ……………
il/elleeut ……………
nouseûmes ……………
vouseûtes ……………
ils/elleseurent ……………

**Conditionnel**
**présent**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………


**passé**
j' aurais
……………
tuaurais ……………
il/elleaurait ……………
nousaurions ……………
vousauriez ……………
ils/ellesauraient ……………

**Infinitif**
présent passé
……… ……………

**Participe**
présent passé
…………… ………/….
…………/tes
ayant ……………

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

MZUNGU mmoja alionekana kumdharau Mbongo, akamwambia waulizane maswali na akishindwa anampatia Sh. 5000 na endapo yeye atashindwa atatoa 100,000.

**Mzungu:** Nchi ipi ilishindwa kwenye vita kuu ya kwanza ya Dunia?

**Mbongo:** akashindwa akatoa 5000 kuashiria hajui.

**Mbongo:** Kitu gani kikienda juu kina miguu minne na kikirudi chini kina miguu mitatu?

**Mzungu:** akafikiria akakosa jibu akatoa 100, 000, kuashiria hajui ila akataka kujua, akauliza ni nini hicho?

**Mbongo:** Akatoa 5000 kuashiria hata yeye hajui!.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mjue mtu aliyefungwa hatua za maisha yake

KARIBU tena msomaji tuendelee kudadavua Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilijaribu kuelezea kwamba hatua za mtu zinaweza kufungwa lakini yeye asitambue, na zaidi akidhani kuwa hali hiyo ni ya kawaida kwake.

Nikasema mtu anaweza kufungwa hatua zake za maendeleo asiweze kusonga mbele akabakia pale pale au akarudi nyuma. Kumbe upo ukuta au mpaka umewekwa mbele yake ili asipenye kwa hali yoyote ile.

Unapotaka kusonga mbele, lazima upende kufundishwa. Kubali kujifunza kujua ni kwa nini hupigi hatua. Wapo watu walipaswa kuwa wakurugenzi lakini leo wanauza mandazi mitaani. Wengine wana matatizo ndani ya familia zao lakini hawajui. Kutojua kuwa una tatizo, hilo ni tatizo kubwa na wala hutafuti ufumbuzi. Huko ni kufungwa ufahamu ili usijitambue.

Watu wengi leo hawatafuti msaada kwa kuwa hawajui. Wapo wenye shinikizo la damu, ugonjwa wa kisukari, kansa, kumbe ni magonjwa waliyokuwa nayo bibi au babu yao. Wameyarithi toka kwa wazazi wao. Pia kuna umasikini wa ukoo unaotesa wengi.

Msomaji wangu, ukweli ni kwamba matatizo yote huanzia ulimwengu wa roho- ule usioonekana, kisha yanajitokeza kwenye ulimwengu wa mwili. Watu wengi leo hawahitaji msaada lakini ukiwaangalia wana matatizo makubwa. Tunahitaji msaada mkubwa sana kujinasua katika maisha yetu.

Kuna watu kila wanapokaribia upenyo, kitu kibaya kinatokea. Wanatembea lakini hawaoni vitu vilivyojificha. Tumwombe sana Mungu atupatie macho ya rohoni tuone yale yanayotokea katika maisha yetu. Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba yapo matatizo mengine yanayowasubiria watu mbele ya safari.

Hebu sasa msomaji wangu msikie kijana huyu, mfano wa mtu aliyefungwa hatua zake za kimaisha. Kila akianzisha kitu akikaribia kupenya, balaa linatokea. Huyu ni mmoja wa wasomaji wa safu hii. Katika ujumbe mfupi simu ya kiganjani anasema hivi;-

"Nimepata namba hii kwenye makala yenye kichwa cha maneneo, 'Zijue dalili za mtu aliyefungwa', niliyosoma kwenye mtandao. Mimi nina matatizo kana ulivyoeleza, na muda mrefu nimekosa majibu. Naishi Arusha Wilaya ya Karatu. Nina mfululizo wa kuwekeza mamilioni ya fedha, lakini pesa yote inateketea bila faida na mtaji wake unakufa.

"Inatokea Napata mtu wa kuwekeza, hata hivyo matokeo yake napata kashfa ya pesa na hiyo pesa ya mtu tuliyewekeza pamoja kuharibikia mikononi mwangu. Yaani hapa nilipo kila siku natafuta majibu nimekosa.

"Nimekosana na kaka yangu wa kuzaliwa, pesa yake Sh. milioni kumi iliyeyuka mikononi mwangu. Rafiki yangu mmoja naye alinipa Sh.milioni tatu na mwingine Sh. milioni nne, zote ziliyeyuka bila hata faida. Mimi nina uwezo kimkakati kuona fursa lakini mwishoni napata vikwazo vya hasara kubwa.

"Siyo hayo tu, nina duka la pembejeo, hapa dukani hata bidhaa za Sh. laki tano hazifiki na sioni mahali pa kupata mtaji tena. Familia imeniangalia nikiwa na mradi wa ujenzi wa nyumba za biashara, zimeishia kwenye msingi.

"Mbali na kwamba vyuma vimekaza, lakini mimi ninayo akili ya kuona fursa lakini ndiyo hivyo. Sawa na mtu kununua gari na likaungua". Hivyo ndivyo anavyomalizia ujumbe wake kijana huyu mwenye matarajio makubwa kiuchumi lakini amekwama.

Je, wewe una changamoto gani ambayo imekuwa ukuta kwako kimaisha? Kijana huyu anayo nyota kubwa sana ya mafanikio, lakini ipo nguvu inayomzuia. Inawezekana yupo adui kwenye familia au wa nje aliyesimama na kusema hatafanikiwa huyu. Pengine ni rafiki yake waliyezozana au ni wivu tu unamkwamisha kwa njia ya ushirikina au zaidi yawezekana ni roho ya umasikini inayomwandama.

Umasikini ni ngome kubwa duniani iliyoshikilia watu waishi katika mateso makubwa. Roho hiyo imewafanya wanadamu wengi washindwe kufurahia uwepo wao duniani. Mungu amewekeza vitu vingi sana ndani ya mwanadamu.

Lakini ili ujue mtu ni masikini utaona miongoni mwa dalili zifuatazo;- Anakuwa na mzunguko wa madeni. Kila anachokifanya hakikamiliki na kusababisha hasara. Anakuwa na mapato yasiyokidhi mahitaji. Yaani matumizi makubwa kuliko kipato chake. Kutokuwa na uwezo wa kumiliki kitu chochote.

***Msomaji, lazima uwe na nguvu kuvuka ng'ambo yako. Mwenye nguvu siku zote atamshinda aliye dhaifu.Hili nitajadili wiki ijayo. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe tumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Asante Rais Samia hili ni tumaini jipya sekta binafsi

ALHAMISI wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan aliweka tumaini jipya kwa Watanzania wengi hasa jumuiya ya wafanyabiashara na sekta binafsi kwa ujuma, ambao walishakata tamaa kutokana na magumu waliyokuwa wanayapitia.

Kila walipojaribu kusema hawakupata wa kuwatetea kwa kuwa walichotakiwa ni kulipa kodi tu bila kujali kama biashara husika itaendelea kuwa hai au la.

Maelekezo ya Rais Samia yalipokewa kwa furaha kwamba sasa biashara zitarudi hata kama haitakuwa kama zamani, angalau sasa mtu atafungua biashara yake bila woga wa kufungiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kilio kikubwa kilikuwa kutosikilizwa iwapo utakutwa hujalipa kodi za nyuma ulizokuwa unadaiwa na badala ya kuachwa ufanye biashara huku ukiwa na makubaliano na TRA ya kulipa deni husika. Kilichofanyika ni kufunga biashara, kumkamata muhusika na kufungia akaunti zake asiweze kutoa fedha yoyote bali ziendelee kuingia.

Wako waliofunga biashara kabisa, wako walioikimbia nchi na wengine waliopata maradhi na kufariki dunia ghafla na wengine kujimaliza kama yule mfanyabiashara jijini Dodoma.

Wako ambao hadi sasa akaunti zao zimefungiwa na hawawezi kutoa fedha yoyote. Matokeo yake ni waliokuwa kwenye mnyororo wa maisha ya mfanyabiashara huyo yaani waajiriwa, familia na wategemezi wote walijikuta katika maisha magumu. Hali ikiwa hivyo maana yake fedha iliyokuwa inaingia kwenye mzunguko inapungua na wengi wanakosa ajira, fedha na maisha yanazidi kuwa magumu.

Biashara nyingi zimefungwa ambazo serikali ingeendelea kukusanya kodi ikiwamo kodi ya mapato hasa inayotokana na mshahara huku wengi wakiwa na ajira, lakini hali haiko hivyo na sasa mamia ya waliokuwa wameajiriwa wako nyumbani.

Ikiwa watu wengi hawana kazi ya kufanya, maana yake idadi ya wategemezi inaongezeka, umasikini unaongezeka na wengi watapambana kupata mkate wa siku kwa mbinu yoyote ikiwamo kuiba. Hapo ndipo matukio ya wizi na ujambazi yataongezeka.

Hali ikiwa hivyo maana yake waliokuwa wanasomesha watoto shule nzuri watawaondoka na mapato ya shule husika yatatetereka. Matokeo yake wamiliki wa shule watashindwa kulipa mishahara ya watumishi na kodi mbalimbali.

Haitaishia hapo kwa kuwa kuongezeka kwa maskini kutakuwa kero kwa wachache wanaojiweza, hivyo kwa tumaini jipya sasa tutaona biashara zikistawi upya na ile hali ya kudhoofu kwenye sekta binafsi kutapungua taratibu na kwisha.

Hakuna ubishi kuwa serikali haiwezi kuajiri mamia ya wahitimu kwenye vyuo 64 tulivyo navyo nchini bali sekta binafsi ambayo ndiyo injini ya ukuaji uchumi, itaajiri wengi na serikali itapata kodi. Pia itafika mahali ulipaji kodi hautakuwa wa kulazimishwa bali hiari kwa jinsi mambo yanavyokwenda.

Rais Samia ameona kwa jicho lake kuwa kilichokuwa kinafanyika ni kutumia nguvu zaidi kuliko akili. Hali hiyo ilisababishwa na kukosa ubunifu katika kukusanya kodi kiasi cha kuwakamua ng'ombe ambaye ameshakonda hajiwezi hata kula majani.

Nawaza kwa sauti walikuwa wanafikiri nini waliokuwa wanatenda hayo kwamba ingefika wakati idadi ya biashara na kampuni zilizofungwa ingekuwa kubwa kuliko yanayofanya kazi kiasi cha mapato kilichopotea kingekuwa kikubwa kuliko ambacho kingekusanywa.

Watanzania tuna wajibu wa kuijenga nchi yetu na kodi ndiyo itawezesha nchi kusonga mbele na kustawi. Naamini kama sekta binafsi itaimarika, kiwango cha kodi kitaongezeka kwa kuwa watu wataajiriwa na watalipa kodi kupitia ununuzi wa bidhaa na kodi ya mshahara huku mfanyabiashara akilipa kodi zote za serikali.

Kwa tathimini yangu, sekta binafsi ilikuwa inapitia kwenye tanuru la moto kiasi cha kupunguza wafanyakazi kabisa na wengine kufunga, idadi ya waliopo nje ya ajira ni kubwa kuliko walioajiriwa, wengi walikosa mlo wa siku licha ya kuwa na uwezo siku za nyuma.

Sasa Rais Samia ameweka tumaini jipya, hivyo ni wajibu wa mawaziri kumsadia kuhakikisha sekta binafsi inastawi na kutoa mchango wake mkubwa kwenye maendeleo ya taifa.

Janga la corona ndilo lilikuja kupalia mkaa hali iliyokuwapo na madhara yake kwenye biashara ni makubwa. Lakini kubwa ilikuwa TRA ilivyoendesha mambo yake kiasi cha kuumiza wengi badala ya kuwasaidia waendelee kuajiri, kulipa kodi na ada nyinginezo.

Ni muhimu sana serikali ikakabiliana na wakwepa kodi wote na hatua ichukuliwe dhidi yao. Ni muhimu sana Watanzania tukashiriki kuijenga nchi yetu kwa kulipa kodi zote halali kwa wakati kwa kuwa faida yake ni miradi ya maendeleo ambayo tunanufaika nayo kwa pamoja.

Mathalani, ikijengwa shule, zahanati, kituo cha afya, kukiwa na vifaa tiba, miundombinu ya barabara maana yake sote tutanufaika nayo, na hayo yote hayatawezekana bila kulipa kodi ili kuendelea na uendeshaji wa serikali.

Kama Rais Samia alivyosema ni muhimu pia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ya serikali ikawasoma ili iwe rahisi kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi, wizi na uharibifu wowote, ili fedha zote za serikali zikusanywe inavyotakiwa.

Vitabu vitakatifu vimeelekeza kulipa kodi kwamba ya Kaisari mpe Kaisari na ya Mungu mpe Mungu, hivyo tulipe kodi kwa uaminifu.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI



Harusi ya kukumbukwa kati ya Henry Mbilinyi na Bahati Hoza iliyofungwa katika Kanisa la KKKT Dayosisi ya Iringa, Usharika wa Kihesa Novemba 22, mwaka jana



UTUNZAJI VIATU VYA NGOZI

# Tembea ukiwa maridadi zaidi

VIATU ni moja ya vazi ambalo linahitaji utunzaji wa hali ya juu katika vipindi vyote vya mwaka.

Kwa kawaida mtu anapotumia viatu husababisha uchakavu au uchafuzi kulingana na sehemu anazopita au kufanyia shughuli zake.

Katika kipindi cha mvua uangalizi wake unakuwa wa hali ya juu, kutokana na hali hiyo, viatu vinachafuka na kisha kupoteza mwonekano wake.

Kwa hivyo, ni muhimu sana kujua jinsi namna ya kutunza vizuri viatu vya ngozi.

Jambo la kwanza ambalo halipaswi kufanywa kamwe ni kuacha viatu vilivyochafuka kukaa kwa muda mrefu, kwa mfano, ukirudi jioni kinakaa hadi kesho asubuhi.

Hii inaleta ugumu wakati wa kusafisha, viatu huwa vinapoteza mwonekano wake wa kupendeza, lakini pia sura yake.

Vinapochafuka viatu vya ngozi? Hakikisha unasafisha kwa kuviosha na kuvikausha. Baada ya hapo unatakiwa kupaka rangi maalum ili kulainisha.

Hakikisha chumvi na uchafu haipaswi haibaki kwenye viatu. Vinginevyo ubora wake unapungua.

Ili kukausha viatu vyako haraka, unaweza kutumia kitambaa. Chaguo kiwe na umbo la pembe tatu ili kiweze kuingia ndani kwa urahisi.

Ni kosa kubwa kukausha viatu kwa kutumia moto, jiko au oveni.

Hii inapaswa kufanyika tu kwa joto la kawaida. Vinginevyo, viatu vitaharibika.





UREMBO



MAKALIO MAKUBWA

# Urembo unaopendwa, lakini hatari

NI mwonekano mpya, unaowavutia wengi na kusababisha kuwapo na ushindani kwa baadhi ya wanawake waonekane wenye maumbo hayo ya kipekee.

Urembo wa makalio makubwa ni mtindo unaoongezeka umaarufu kwa kasi na kusababisha baadhi ya wanawake kwenda kufanya upasuaji ili kuongeza unene wa makalio yao.

Wanachoamini kwamba kuwa na makalio makubwa na kiuno chembamba inamfanya kuwa na umbile mzuri la kupendeza.

Lakini wasichokifahamu, urekebishaji wa kiungo hiki ikiwamo upasuaji na kuongeza unene unaofanywa katika hospitali za nje una hatari nyingi kuliko faida yake.

**ATHARI MBAYA**

Wanaofanyiwa upasuaji wa aina hii wana uwezekano mkubwa kupata matatizo ya moyo, kuongezeka kwa mafuta mwilini na pia kifo.

Leah Cambridge kutoka Leeds Uingereza, alipata matatizo ya mshtuko mara tatu baada ya kudungwa sindano ya ganzi katika kliniki moja katika mji wa Izmir, wakati akifanyiwa upasuaji.

Kinachofanyika ni kufanyiwa upasuaji wa kuongeza makalio kwa kutoa mafuta kutoka tumboni na kuwekwa katika makalio.

Mrembo huyo alifanya upasuaji baada ya kukerwa na mafuta mengi katika sehemu yake ya tumbo baada ya kupata watoto.

Kuna wasanii mbalimbli maarufu ambao wamefanyiwa upasuaji wa aina hii, akiwamo Kim Kardashian, Cardi B na mdogo wake Khloe.

Kwa mfano Joy Williams alifariki dunia baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuongeza makalio yake mjini Bangkon nchini Thailand.

Vidonda vilivyotokana na upasuaji vilipata maambukizi na alifariki wakati akidungwa sindano ya ganzi.

Upasuaji wa kuongeza makalio hauonekani kuwa hatari zaidi ya aina nyengine zozote za upasuaji, kulingana na daktari wa upasuaji wa urembo Bryan Mayou.

Hata hivyo, hatari yake ni baada ya kufanywa na madaktari ambao hawajahitimu nje ya kliniki kama wengi kutoka mataifa maskini wanapokimbilia.

Iwapo mafuta yataingizwa katika tishu ya sehemu ya makalio, kuna hatari mafuta hayo kuingia katika mishipa mikubwa ya damu.

Mafuta hayo yanaweza kupita katika mishipa ya damu na kisha kuingia katika mapafu na kusababisha kifo.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

FURAHIA PASAKA



# 'Dessert ya Strawberry'







SIKU ya sikukuu kama leo, unapokuwa na familia ni vizuri ukapata mlo utaosindikizia chakula chako.

'Dessert ya Strawberry', Apple na Ndizi ni mlo ambao utakufanya wewe na familia yako mfurahie vyema mara baada ya kula chakula kizito cha sikukuu.

Unaweza kuandaa 'dessert' hii kwa kutumia tunda moja, hasa strawberry au unaweza kuchanganya matunda tofauti ili kupata ladha na virutubisho zaidi.

**NAMNA YA KUANDAA**

Andaa matunda kwa kuosha na kisha kuyakata vizuri.

Kata strawberry vizuri na weka kwenye bakuli (au chombo unachotengenezea dessert yako).

Kata ndizi kwenye vipande vidogo na uchanganye kwenye strawberry.

Menya na kisha kata apple vipande vidogo vidogo, changanya pia matunda mengine kwenye bakuli tofauti, weka maziwa kiasi, changanya sukari na kisha koroga ili sukari ipate kuyeyuka. Hakikisha maziwa ni ya baridi, maana hiki ni kinywaji baridi.

Weka matunda kwenye maziwa, koroga kiasi na ongeza Vanilla ili kuipa ladha na harufu tamu dessert yako.

Unaweza kuacha mchanganyiko kwa muda mfupi kwenye jokofu, au unaweza kula moja kwa moja.

Unaweza pia kuchanganya parachichi au nanasi kwenye mchanganyiko ili kuongeza utamu.

Furahia mlo wako wa sikukuu kwa kujilamba na dessert yako.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Hizi ndizo kero za madalali kwa watu wanaotaka kupanga



Ni kawaida watu wengi wanapokuwa wanatafuta nyumba za kupanga kwa ajili ya makazi, biashara au kununua hutumia madalali ambao ni wabobezi katika eneo hilo.

Pamoja na kupendelea kuwatumia madalali hao, wengi wao wamekuwa wakiwalalamikia kwamba wanawakera.

Na leo tunaangazia sauti za watu hao ambao wanalalamikia kero wanazokutana nazo kwa madalali hao.

Wa kwanza anasema: "Kiukweli nakerwa sana na madalali wa nyumba za kupanga. Kwanza nataka kujua hii sheria yao ya kuwapa kodi ya mwezi mmoja wanapokutafutia nyumba, imepitishwa na nani, na je, wanalipa kodi kwa serikali tunayoowapa hiyo kodi ya mwezi mmoja?

"Na hii sheria ya kupelekwa kwenda kuona nyumba au chumba kwa Sh.5, 000 au 10,000 nani kaipitisha? Nimeandika hivi kwa sababu usumbufu tunaoupata wakati wa kutafuta nyumba ni mkubwa mno. Madalali wengine ndio wamekuwa kama wenye nyumba, hadi bei za nyumba wanabadilisha.

"Wanawashauri wenye nyumba kubadilisha au kuongeza kodi ili wapate fedha kubwa. Ikumbukwe kwamba dalali ni daraja la watu wawili, mwenye nyumba pamoja na mpangaji, lakini inakuwaje jukumu la kulipa hiyo fedha ya mwezi mmoja lisiwe la wote wawili, kwa nini aachiwe mpangaji peke yake?

"Ama walipe wenye nyumba tu na si wapangaji maana wao wanahangaika sehemu ya kujihifadhi. Maskini ya Mungu unakuta alikotoka amefukuzwa kwa kushindwa kulipa kodi ila cha ajabu zaidi anakokwenda anatakiwa alipe kodi ya miezi mitatu hadi sita na kodi ya dalali juu pamoja na Sh. 5,000 au 10,000 kila nyumba anayopelekwa kuiona."

Mwingine anasema miongoni mwa kero zinazomtesa kutoka kwa madalali ni kutokupenda kusema ukweli.

"Lipo tatizo la uongo kwa madalali wengi. Unamweleza kwamba nataka nyumba ya aina fulani, anakwambia njoo ninayo, ukimwomba akutumie picha, anakwambia niko mbali kidogo na sijapiga picha, ukija utaiona mwenyewe lengo tu apate hiyo Sh.10,000 yake . Utaambiwa nyumba iko karibu na barabara. Sasa ukienda utajuta kumfahamu, kiukweli inakera sana sana sana.

MPANGILIO

## Dondoo muhimu namna ya kuchagua taa za kupamba sebule yako




**1:** Chagua taa ambazo hazina mwanga mkali, hakikisha zinaendana vizuri na rangi ya sebule yako.

**2:** Unaponunua hakikisha unachukua zenye ubora ili kukuepusha na tatizo la kubadirisha kila wakati na kukuongezea gharama.

**3:** Kama dari ipo chini sana, weka taa za kutumbukia ndani au taa za sakafuni ili kuhakikisha mwanga hauwezi kuharibu muonekano.

**4:** Chagua taa yenye marembo yasiyochosha, kama urembo una ukubwa kiasi weka ukutani kama sentimita 10 kutoka darini.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
KAMA ZINA-NIINGIAINGIA SENTESI ZAKO!
...MAMA AKIKU-TUMA KITU LAZIMA AULIZE CHENJI!... BANIA UONE!
NINACHOTAKA MIMI UNIHAKIKISHIE KAMA UTAFANYA KAMA NILIVYOKUAGIZA AU NIKUSHUGHUKIE?
HIVI NI NINI KINAKUPA JEURI YA KUJIAMINI KIASI HICHO?
MWANAUME MWENZANGU HILO SIO SWALI SOMA ALAMA ZA NYAKATI!
NAONA UNA-USHUHUDIA MZIKI MPYA...
KWA REDIO IPI?
MOTO WA MAMA...
KAKA KAMA NAKU-FANANISHA!... SIJUI TUMETOKA KIJIJI KIMOJA?
KAWAAMBIE YULE BWANA HAJUANI NA WAZEMBE...
BABA, MOTO NI ULE ULE HAUZIMWI KWA KUPULIZA!
CHUMA BADO KIPO
TUSIOPEPESA MACHO MAKAZINI HATUNA BUDI KUTEMBEA HIVI...
WE HAYA WE!
TOFAUTI NA BABA... MAMA AKIKUCHOMA SINDANO INAINGIA HUKU UNABEMBE-LEZWA...
KUNA UNACHO-KUSUDIA KUSEMA... WE SEMA WAZI WAZI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
... MTETEZI WA MWIZI ZIRAILI...

# Wawili wauawa shambulio bunge la Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

WATU wawili wamekufa katika tukio la dereva wa gari kufanya shambulizi la kuwagonga maofisa wawili wa polisi karibu na majengo ya bunge nchini Marekani Capitol.

Waliofariki dunia ni askari polisi ambaye alipata majeraha mabaya na dereva wa gari hilo ambaye alipigwa risasia katika tukio hilo.

Mshukiwa wa shambulizi hilo, alivurumisha gari dhidi ya askari polisi wawili waliokuwa wakishika doria katika majengo ya bunge ya Marekani yaliyoko Capitol mjini Washington DC, na baadae alipigwa risasi na polisi.

Shambulizi hilo limefanyika karibu na mahali ambapo wafuasi wa Donald Trump waliingilia majengo hayo Januari 6, mwaka huu.

Maofisa wa polisi walisema gari hilo liliendeshwa kwa kasi kwa kuwalenga polisi liligonga vizuizi vya usalama, kisha mshukiwa aliyekuwa akiliendesha akatoka nje akiwa amebeba kisu mkononi na kukimbia kuelekea kwa polisi hao. Mshukiwa huyo alikaidi amri kutoka kwa polisi wa usalama na ndipo wakampiga risasi na alifariki wakati akipatiwa matibabu hospitalini.

Askari polisi waliojeruhiwa pia walikimbizwa hospitalini na mmoja alifariki.

"Kwa masikitiko makubwa tunatangaza kuwa ofisa wetu mmoja amefariki kutokana na majeraha," alisema Yogananda Pittman, Kaimu Mkuu wa Polisi wa Capitol.

Aliwaomba Wamarekani kumwombea marehemu "Tafadhali mkumbukeni kwenye maombi yenu,"

Kisa hicho kilitokea takriban mita 90 kutoka katika lango la Kaskazini la kuingia majengo ya bunge upande wa baraza la seneti, ambalo hutumika na maseneta pamoja na maofisa wa polisi siku za kazi. Rais wa Marekani, Joe Biden, ambaye hayuko mjini Washington alisema yeye pamoja na mke wake Jill Biden, wamesikitishwa na shambulizi hilo.

"Jill pamoja na mimi tulisikitishwa kusikia kuhusu shambulizi katika eneo la kizuizi cha usalama kwenye majengo ya bunge ambalo limesababisha kifo cha ofisa wa polisi, William Evans wa kikosi cha polisi cha Capitol, na pia kusababisha mwengine kulaza hospitalini,"alisema Biden.

Aliongeza "Tunatuma salamu za rambirambi kwa familia ya Evans na yeyote anayehuzunika kufuatia kifo chake."

Maeneo hayo ya majengo ya bunge yamefungwa na usalama kuimarishwa.

Aidha polisi walisema wameanzisha uchunguzi dhidi ya kisa hicho.

**DW**




Polisi wakichunguza gari lililotumika katika tukio la uvamizi kwenye jengo la bunge la Marekani jana **(PICHA: DW)**

# 550 wapoteza maisha Myanmar

**YONGON, Myanmar**

KUNDI la kutetea haki za binadamu nchini Myanmar limesema idadi ya watu waliofariki kutokana na kamata kamata inayofanywa na jeshi imefikia 550.

Watu waliofariki dunia ni pamoja na watoto 46 tangu kuanza kwa maandamano baada ya kufanyika mapinduzi ya serikali Februari mosi, mwaka huu.

Kundi hilo limesema takriban watu 2,751 wamekamatwa au kushitakiwa. Hata hivyo vitisho vya vurugu na kukamata waandamanaji vimeshindwa kuwadhibiti waandamanaji wanaojitokeza barabarani kila siku nchini humo.

Waandamanaji hao wanalitaka jeshi hilo liachie madaraka na kurejesha utawala wa kiraia uliochaguliwa kwa njia ya kidemokrasia.

Ijumaa iliyopita polisi waliokuwa wamevalia nguo za kawaida walikamata watu watano baada ya kuzungumza na mwandishi habari wa shirika la kimataifa la CNN katika soko la Yongon.

**DW**

# Iran yaweka matumaini mapya mazungumzo ya nyuklia

**TEHRAN, Iran**

IRAN ina imani na mazungumzo kuhusu makubaliano ya nyuklia na viongozi wa mataifa yalio na nguvu duniani yanayotarajiwa kufanyika wiki ijayo mjini Vienna.

Kiongozi wa shirika la nishati ya atomiki nchini Iran, Ali Akbar Salehi, alisema wanakaribia kutoka kwenye mkwamo kwa sababu ajenda za majadiliano haziendeshwi kisiasa bali kwa kuzingatia masuala ya kiufundi na kimalengo zaidi.

Siku ya Ijumaa kulikuwa na mkutano kwa njia ya video kati ya Iran na mataifa matano yaliyobakia katika makubaliano hayo ya nyuklia ambayo ni China, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza na Urusi.

Wote walikubaliana juu ya mazungumzo hayo ya kuuokoa mpango wa nyuklia wa Iran na uwezekano wa Marekani kurejea katika makubaliano hayo.

Makundi ya wataalamu watakutana mjini Vienna nchini Uswisi siku ya Jumanne wiki ijayo, na kuhudhuriwa na wawakilishi wa Marekani.

**DW**

# DRC, Rwanda kushirikiana kijeshi

**KINSHASA, DRC**

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imesema vikosi vyake vya jeshi vitapanua ushirikiano wa kijeshi na nchi zilizo katika ukanda huo.

Siku za hivi karibuni, maofisa wa usalama wa DRC na nchi jirani ya Rwanda, waliongeza kasi ya mikutano ya majadiliano tangu Rais Felix Tshisekedi, aingie madarakani.

Lengo la ushirikiano huo ni kukomesha vikundi vyenye silaha ambavyo yamekita mizizi kwenye maeneo ya mipaka ya nchi hizo mbili.

Taratibu za ushirikiano hazijawekwa wazi na hii inaibua maswali mengi kwa mashrika ya kiraia na baadhi ya viongozi waliochaguliwa.

Hata hivyo jeshi la nchi hiyo (FARDC) lilielezea uamuzi huo ulitokana na nia ya wakuu wa nchi za ukanda huo kukapambana dhidi ya ukosefu wa usalama, unaosababisha vikwazo vya uimarishwaji wa uchumi wa nchi husika.

Kulingana na jeshi la DRC, wajumbe mbalimbali kutoka nchi hizo wameanza kukutana.

Hadi sasa, Rwanda na DRC pekee ndio wanaendelea katika suala hilo la muungano wa kijeshi.

Katikati ya mwezi Machi, Mkuu wa majeshi ya Rwanda, alifanya ziara nchini DRC na kuandaa mpango wa pamoja wa utekelezaji wake.

Kwa upande wa wajumbe waliochaguliwa na mashirika ya kiraia, wana hofu kwamba mpango huo utapelekea operesheni za pamoja za kijeshi mashariki mwa nchi hiyo eneo ambalo lina ukosefu wa usalama.

**RFA**

SAFU

MAKALA

# TUSIPOBADILI FIKRA ZETU HATUTABADILI MATENDO YETU



Na Magabilo Masambu

**Tukipunguza matumizi ya nguvu katika kutatua mambo yetu badala yake tukatumia akili na maarifa, tutapiga hatua kubwa. Yako maeneo mengi ambayo yanahitaji mabadiliko ili Tanzania ya Mwalimu Nyerere yenye umoja na mshikamano irudi.**

NI ukweli kwamba matendo yetu ya kila siku hutokana na fikra zetu. Fikra zetu zinaweza kuwa njema au ovu pia hautakuwapo ubishi katika hilo. Yako matendo tunayotenda kwa kufikiri vizuri lakini yapo matendo yanayotokana na fikra mbovu pia.

Yako matendo mengine ambayo tunayatenda bila kufikiri kabisa. Unaweza kusikia mtu anasema ametenda jambo bila kufikiri na mara nyingi mambo yanayotendwa bila kufikiri huwa mwisho wake ni majuto. Matendo haya mara nyingi hutokana hasira, mihemuko, jaziba, kiburi na mambo mengine kama nayo.

Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa hotuba yake ya kwanza kabisa baada ya kuingia katika nafasi hiyo, pamoja na mambo mengine, alitoa matumaini makubwa kwa Watanzania akisisitiza umoja, amani na mshikamano na kusisitiza kwamba yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Ni jambo jema na Watanzania wakalipokea kwa shangwe na matumaini ya kujenga tena umoja wetu bila kubaguana kwa misingi ya vyama, makabila au dini.

Maneno hayo yatakuwa na maana tu, ikiwa yataendana na matendo ya viongozi wenye dhamana yakianzia kwa Rais mwenyewe mpaka ngazi ya chini. Jambo hili halitawezekana kama hatutabadili fikra na mtazamo baina yetu wenyewe. Maneno si tatizo, tatizo ni kwa kiasi gani matendo yetu yanaakisi maneno yetu. Maandiko matakatifu yanasema imani bila matendo imekufa, vivyo hivyo maneno bila matendo yenye kufanana na maneno hayo yatakuwa yamekufa.

Baada ya hotuba ya Rais, pamekuwapo baadhi ya viongozi katika hotuba na mazungumzo yao, inaonyesha bado hawajakubali kutoka kule tunakotaka tutoke, inawezekana ama hawataki kubadili fikra zao au hawajaelewa dira ya Rais. Kuna uwezekano wa wao kuendeleza matendo yale yale yasiofanana na maneno ya matumaini kwa Watanzania yaliyotolewa katika hotuba ile.

Wakati mwingine fikra ni imani. Nataka niamini kwamba pengine bado ni mapema sana, japo waswahili wanasema nyota njema huonekana asubuhi. Si dhambi watu kuwa na mawazo tofauti ya yako, ndivyo tulivyoumbwa, hatuwezi kufikiri sawasawa hata mapacha wanaofanana huwa wana fikra tofauti kwa nini liwe tatizo mtu kufikiri tofauti na mawazo yako?

Kuna fikra mbovu kabisa kuwahi kutokea katika taifa hili la baadhi ya watu kujiona Watanzania na wengine siyo, wanahaki wengine hawana, wanafahamu wengine hawafahamu. Unapopata fursa ya kuwa kiongozi, ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu. Si kwamba unastahili sana kuliko wengine hata kama unaamini nafasi hiyo umeipata kwa njia za kiganga hata waganga nao wanamwomba Mungu awaletee wateja!

Nafasi ya madaraka lazima itumike kustawisha maisha ya watu na si kuwadidimiza. Tukipunguza matumizi ya nguvu katika kutatua mambo yetu badala yake tukatumia akili na maarifa, tutapiga hatua kubwa. Yako maeneo mengi ambayo yanahitaji mabadiliko ili Tanzania ya Mwalimu Nyerere yenye umoja na mshikamano irudi.

Eneo moja ambalo linahitaji mabadiliko makubwa ya fikra ni juu ya ukusanyaji wa kodi. Tunafahamu kwamba nchi haiwezi kujindesha bila kodi lakini kodi isiwe chanzo pekee. Kufanya hivyo ni kufanya mapato ya kodi kuwa kama pesa za vikoba, ambazo watu hukopeshana bila kuzalisha, yaani unakusanya kodi kwa wafanyakazi kisha unawalipa tena mwisho wa mwezi.

Wizara za fedha, kilimo, biashara na viwanda nashauri mkae pamoja kuona ni kwa namna gani mtashirikiana ili kupata fedha za kigeni kupitia uuzaji wa bidhaa tunazozalisha hapa kwetu, badala ya kuwakamua wananchi kwenye kodi pekee. Walipakodi wanatakiwa kuwekewa mazingira ya kupenda kulipa kodi bila vikosi vya polisi na maofisa wa TRA kuwaendea na bunduki.

Eneo la pili ni kuhusu vyama vya siasa, tunatumia nguvu na muda mwingi kuhangaika na mambo ambayo yapo kisheria. Nafikiri pia tuna haja ya kubadili fikra zetu. Siku hizi limekuwa jambo la kawaida kwa kiongozi yeyote wa serikali akitoa hotuba lazima azungumzie vyama vya upinzani!

Nafikiri si sahihi na si lazima na nataka niwahahikishie viongozi wa serikali kwamba mkiweza kutoa hotuba zenu bila kuzungumzia masuala ya upinzani au uchama ukosoaji utapungua kwa kiwango kikubwa sana.

Njia mojawapo ya kuleta amani na maelewano ni kupuuza baadhi ya mambo. Mtu ukishakuwa Rais au waziri, ikiwezekana hata mavazi ya chama chako yaweke pembeni kwa muda ili kuleta ushirikiano kwa sababu wote kwa pamoja tunahitajiana.

Mwisho, ni imani yangu kwamba tutapata suluhu ya mambo mengi chini ya mipango mizuri na maendeleo hayatakuwa majaliwa tena bali yatakuwa ya uhakika chini ya uongozi mzuri wa Rais Samia, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa pamoja na serikali yote kwa ujumla.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kiti cha baba hakikaliwi, redio hadi arudi*



Na Adam Fungamwango

**Nilizoea mjini tunakula tukiwa tumekaa kwenye viti, wakubwa na wadogo. Mara chache sana ndiyo chini na hasa tukila na kinamama. Kwenye viti ni wakati wa kula na baba au wageni.**

NAKUMBUKA katikati ya miaka ya 1980, nikiwa Mpanda mkoani Rukwa wakati huo kabla ya kuitwa Katavi.

Ulifika wakati wa kula. Tukaitwa watoto wote kwenda kupata chakula cha mchana. Chakula kiliwekwa kwenye kigoda na vigoda vingine vichache vikiwa pembeni. Nilikuwa sielewi utamaduni au taratibu za huko kwa sababu ilikuwa ndiyo siku ya kwanza kufika huko na mama yangu tukitoka Dar es Salaam, kwenda kusalimia.

Watoto wenzangu wote walikaa chini. Wakanawa na kuanza kula. Babu yangu mzaa mama na mwenzake mmoja wakakaa kwenye vigoda. Mimi kwa sababu sielewi kitu nikavuta kigoda kimoja na kukaa. Kilichotokea ni kwamba babu alinifokea na kunitaka nikae chini mara moja. Nikatoka kwenye kigoda haraka na kukaa chini.

"Mambo ya kwenu mjini usiyalete hapa. Hapa watoto wanakaa chini na watu wazima ndio wanakaa kwenye vigoda. Hizo ndizo taratibu za kwetu. Mtoto hawezi kukaa kwenye kigoda awe sawa na mtu mzima," Babu alinifafanulia.

Tangu siku hiyo nikawa natii amri bila shuruti hadi niliporejea Dar es Salaam na mama. Hii ilionyesha kuwa zamani kulikuwa na aina fulani ya maisha, utamaduni na taratibu zilizoendana na sehemu na mazingira. Baadhi zilitofautiana na zingine zilifanana.

Nilizoea mjini tunakula tukiwa tumekaa kwenye viti, wakubwa na wadogo. Mara chache sana ndiyo chini na hasa tukila na kinamama. Kwenye viti ni wakati wa kula na baba au wageni.

Hata hivyo, bado kinababa walikuwa na viti vyao. Hivi ni vile vya kupumzikia nje wakati wanapunga hewa, au wanapumzika. Vingi vilikuwa vinatengenezwa kwa mbao. Kuna vya kukunja na vile ambavyo wenyewe wanaviita 'viti vya uvivu'. Ni viti ambavyo vilikuwa vinatumiwa na kinababa peke yao. Hata kwa bahati mbaya, huwezi kukuta hata mama ameamua kukikalia, achilia mbali mtoto.

Tayari valishatengenezwa mazingira kuwa ni kiti cha baba, hivyo watoto pamoja na utundu wao wote, hawakuvigusa. Na ikitokea bahati mbaya ikawa hivyo, adhabu yake ni viboko.

Wazazi wa zamani walikuwa hawamnyimi mtoto viboko. Kosa la kujirudiarudia, liliweza kusababisha kucharazwa bakora kila siku.

Viti hivi vilitumiwa kina baba wanaporudi kazini, anatoka nacho kwenda nje, kwenye kivuli, upepo na tulivu, anakuwa amevaa kaptura au msuli wake, juu ana 'singlendi', mawani ya macho na gazeti lake, atakaa hapo hadi atapochoka, au kuitwa ndani kwenda kula chakula.

Hapo mtoto kama umefanya kosa lolote, ikiwemo kutokwenda shule, ukimuona amekaa hapo, hupiti hadi aingie ndani, maana unahofia kuitwa na kuanza kuulizwa maswali ambayo yanaweza kukutia hatiani.

Wakati watoto wa sasa wanakaa sebuleni wakiwa wana uhuru wa kuchagua chaneli yoyote ya televisheni na kuangalia hata wazazi wao wakiwepo, zamani haikuwa hivyo.

Redio yenyewe kusikiliza hadi baba awepo. Kitendo chochote cha kutafuta redio ilipo na kuifungulia mwenyewe hayupo ni kosa kubwa ambalo linaweza kusababisha adhabu ya viboko.

Halafu walikuwa na uwezo wa kuweka sehemu ambayo hata ukiishika tu na kuangalia, ukairudisha tena akirudi anajua kuwa kuna mtu ameigusa redio yake. Na hadi mtasema ni nani.

Yeyote anayetaka kusikiliza redio ni lazima amsubiri baba arudi, afungulie ndipo watoto mkae msikilize. Na hata kusikiliza kwenyewe si vipindi vyote. Kuna vipindi ambavyo watoto wanaambiwa waondoke kwani haviwahusu.

Wako watoto waliokuwa watundu zaidi ambao walikuwa na uwezo wa kufungua, kusikiliza na kurudisha bila baba kujua.

Hapo sasa kuna kuzidiana akili, kati ya baba na mtoto. Ukimkuta baba mwingine akiona betri zinaisha wakati hajatumia kwa muda mrefu, anaanza kuhisi kuna mtu huwa anafungulia redio yake.

Atakachofanya ni kuzigeuza betri. Kama redio ya betri nne, kati ya kati utageuzwa ielekee upande mwingine, hivyo yoyote atayeifungua itaendelea kunyamaza tu. Ni udadisi wa hali ya juu tu ndiyo unaweza kugundua kuwa betri moja limegeuzwa, vinginevyo unaiacha na kuendelea na shughuli zako.

Hii haikuwa na maana kuwa wazazi wa zamani walikuwa na roho mbaya na hawapendi watoto wao, la hasha.

Ilikuwa kuwajenga kwenye utamaduni wa nidhamu na adabu. Pia ikumbukwe kipindi hicho waliokuwa si wengi waliokuwa na uwezo wa kumiliki redio.

Kwa sababu hiyo ilikuwa ni kama kuilinda ili watoto wasiharibu. Hata upatikanaji wa betri nao ulikuwa wa mbinde. Unaweza kuwa na redio, lakini huwezi kupata betri hata miezi miwili. Baba akaishia tu kubondabonda betri zilizopo na kuzianika juani ili redio ipate kuongea hata kwa dakika 30 tu.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora, Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi zilimfanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini alimteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia sehemu ya mwisho ya kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu - 16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NASHUKURU sana wanawake ninyi wenye akili na busara. Ingekuwa wengine wangegombana. Ester usingekuja kumtetea Neema hapa kwa sababu yeye ndiye aliyesababisha uachwe na akaolewa yeye. Na Ester ungeweza kumfanya chochote mtoto Neema kwa hasira ya kutelekezwa, lakini ulimlea kama mtoto wako, hadi ulipomrudisha kwa mama yake.

"Lakini nilichofurahi sana kumbe dhamira ya kumteka kwa kumdhuru, ilikuwa kumlazimisha baba yake aje muelewane, ila tu ilishindikana kwa sababu alikuwa amebadilisha namba za simu kwa kusajili laini nyingine. Hata Neema ungeweza kumchukia Ester kwa sababu ndiye aliyesababisha kutekwa mtoto wako Diana. Na amesababisha ndoa yako leo iko shakani na una talaka mkomoni. Hamkujali yote.

"Ninyi ni wanawake mashujaa na mfano wa kuigwa. Ingekuwa wanawake wengine ingekuwa nongwa. Kila mmoja angetaka kujifanya mjuaji na ni zaidi na mwenzake. Mimi nadhani tu itoshe kusema kila mmoja afanya anachojisikia kufanya.

"Wakubwa zangu mimi nimemaliza. Alinitekeza, naendelea na maisha yangu. Ndugu yenu ameoa, siwezi kufanya chochote. Na hata kama kwa sasa asingekuwa na mke, siwezi kurudiana naye tena," alisema Ester akinyanyuka, tayari kwa kuondoka.

"Nisubiri tuondoke wote shoga." Ilikuwa sauti ya Neema. Pamoja na kwamba kila mtu anatambua kuwa lengo la mkutano ule ile talaka aliyopewa na mumewe. Lakini hawakudhani kama angeondoka mapema kiasi kile, au mara baada ya kikao.

"Mimi pia naondoka. Nina talaka mkononi. Kama alinipa kimakosa au alikuwa na hasira sijui, lakini kwa yote ambayo ameyafanya, sina haja ya kuishi na mwanamume kama huyu. Kama alimtelekeza mwanamke akanioa mimi, atashindwaje huko mbele ya safari asinitelekeze na mimi? Hapa tu tayari alishaniona ni kahaba, nimesababisha mtoto atekwe. Shoga, ngoja nimvalishe Diana twende zetu."




Walitoka nje ya geti. Kwa mbali Neema aliliona gari lilikuwa limepaki. Wala hakujiuliza mara mbili kuwa ndilo lililmleta Ester nyumbani kwake alipompigia simu na kumuekeza kuwa aje kwenye kikao hicho kwa ajili ya kuumaliza utata. Lilikuwa la Jerry.

**Neema aliahidi atamlinda kwa gharama yoyote ile. Lakini na yeye akaomba asaidiwe kitu kimoja. Alijua ataulizwa alimpata vipi mtoto kirahisi. Alijua itamletea matatizo. Lakini alimwomba Ester kumsaidia pindi atakapohitaji msaada.**

*****************************

Alikuwa ameteremka kwenye gari kwenda kupoza koo kwa soda. Alikuwa amemleta Ester. Ulikuwa mpango uliowekwa na yeye mwenyewe, Ester na Neema. Baadaye tukio lile, Ester yeye aliomba asitajwe na ifanyike kila njia asikamatwe yeye, mjomba wake na hata rafiki yake kwa kosa la kumteka mtoto kwa sababu hawakuwa na nia mbaya.

Neema aliahidi atamlinda kwa gharama yoyote ile. Lakini na yeye akaomba asaidiwe kitu kimoja. Alijua ataulizwa alimpata vipi mtoto kirahisi. Alijua itamletea matatizo. Lakini alimwomba Ester kumsaidia pindi atakapohitaji msaada.

Ndipo lipotokea siku ambayo alihitaji. Baada ya kupewa talaka, pamoja na kwamba alisikitika, hakutaka kuondoka bila ndugu za pande zote mbili kujua ukweli wa mambo.

Ndipo alipoitisha kikao na kumpigia simu Ester ili aje amalize utata, kwani angeongea mwenyewe ingeonekana anajitetea tu. Lakini ilikuwa pia kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Si tu kuthibitisha kuwa aliyemteka mtoto Diana hakuwa hawara wa Neema kama ilivyovumishwa, lakini pia kuonyesha kuwa kisa hicho kilikuwa kinyume chake.

Ni kwamba aliyemteka Diana, ni mzazi mwenzake Ben ambaye alimtelekeza. Kibao kiligeuka. Na hao wote wawili hawakufahamiana kabla. Walifahamiana kwa bahati nasibu sana, kwa msaada wa Jerry.

Pia ndiye alimleta Ester pale, baada ya maelezo Neema mwenyewe.

Wakati anarejea, aliwaona Ester na Neema wakitoka. Ester alikuwa amembeba Diana.

"Na wewe unakwenda wapi?" Alimuuza Neema.

"Naenda kwa Ester. Nimeachwa, unafikiri nitaenda wapi? Nakwenda kwa shoga yangu."

Suala ya kuachwa haikuliwa kwenye kichwa cha Jerry. Pamoja na kumpenda, hakutegemea kuachwa kirahisi namna ile.

"Unasemaje?" Aliuliza.

"Hujasikia. Nimechwa na talaka nitakuonyesha tukiwa ndani ya gari."

"Neema na Jerry. Mimi nashukuru sana kwa kampani mliyonipa. Sikutegea hili." Ester alisema baada ya gari kutia moto.

"Usijali. Wewe ndiye umenifanyia kitu kikubwa sana. Nimeondoka pale bila ya aibu wala fedheha. Nimeondoka kama shujaa, na fedheha nimeacha na mtu aliyetaka kunipa aibu." Neema alijibu.

"Sasa tunaenda wapi? Ubungo au kwangu Chang'ombe?" Ilikuwa zamu ya Jerry kuongea wakati gari likiwa limesimama kwenye foleni.

"Mimi naona tupeleke Ubungo kwanza. Nahitaji kupumzika kwa siku tatu kwanza kwa shoga yangu Ester ndiyo mambo mengine yaendelee."

"Jerry una haraka hivyo?" Alidakia Ester ambaye tangu siku nyingi aliona dhahiri penzi la Jerry na Neema kwenye mioyo yao, lakini likiwa limefungwa na ndoa, ambayo kwa sasa haipo. Anajua kuwa zamani alikuwa mpenzi wa Jerry akiwa chuoni, lakini liliyayuka baada ya wazazi wake kumhamisha.

Pamoja kukutana baada ya miaka mingi, lakini hakuona kama Jerry ana mapenzi tena kwake. Hivyo wala hakutaka kulazimisha. Aliliacha penzi la Jerry na Neema liendelee. Na alijua kwa sasa Neema yuko huru, hivyo litachanua kama ua lilotiwa mbolea.

"Usiwe na wasiwasi Jerry. Mimi sasa si mke wa mtu tena. Na najua unanipenda. Yote hata yote umeyafanya kwa ajili yangu. Mimi niko huru. Talaka ni hii hapa."

Neema alikuwa amekaa mbele na Jerry aliyekuwa akiendesha gari, Ester nyuma akiwa amembeba Diana.

Walishindwa kujizuaia, wakajikuta wamekumbatiana kabla gari halijaondoka kwenye foleni.

"Nakupenda na nitaendelea kukupenda daima. Nitakuoa Neema."

" Hata mimi nilijua unanipendaKazi kwako tu kaka. Samaki ni wako, utajua mwenyewe kama utamkaanga, utamchemsha au kumla chukuchuku." Neema alimwambia Jerry na kusababisha kicheko ndani ya gari.

**MWISHO**



# MOSHI MWEUSI PENZI LA HARMONIZE, KAJALA

KIVUMACHO huwa hakidumu, ndivyo mapenzi ya wasanii Harmonize na Kajala Masanja yalivyokuwa yakivuma kama kimbunga, lakini ghafla yamekatika kama umeme.

Sasa ndio habari ya mjini kwani katika mitandao ya kijamii mjadala umekuwa kufika mwisho wa penzi hilo, huku viashiria vikionyesha wawili hao hawapo tena kimahaba.

Kajala Masanja amefuta picha zote alizowahi kuposti akiwa na Harmonize kwenye mtandao wa Instagram, kisha kumuondoa urafiki kwenye mtandao na kuandika ujumbe wa Kiingereza uliotafsirika kama

"Usimuumize mtu kwa ajili ya sababu zako binafsi"

Uhusiano kati ya Harmonize na Kajala uliibuka kwa kasi na kuwavutia watu wengi hadi kufikia hatua ya kuchorana tattoo.

## Jitu Baya alia 'Tutawakumbuka'

RAPA anayekuja kwa kasi, Jitu Baya, ametambulisha singo yake mpya maalum kwa ajili ya kuwaenzi viongozi mbalimbali walioongoza Tanzania.

Amesema wimbo huo unaoitwa 'Tutawakumbuka' ameutunga kwa ajili ya kutumika kipindi kirefu kwani unaelezea kazi nzuri zilizoachwa na viongozi hao wakati wakipigania maendeleo ya nchi.

"Sikutaka kutunga wimbo kwa ajili ya muda huu wa kuomboleza kifo cha Rais wetu mpendwa Dk. John Magufuli, nataka uchezwe kila wakati tunapowaenzi viongozi wetu wote waliotangulia mbele ya haki bila kuonekana umepitwa na wakati," amesema Jitu Baya.



## Steve kumbe kifurushi kilikutoa jasho?

MSANII wa filamu Steve Nyerere, ni miongoni mwa Watanzania waliohamanika na gharama kubwa ya vifurushi vipya vya data vilivyotangazwa na kampuni mbalimbali za simu.

Hata hivyo, serikali imetangaza kusitisha matumizi ya vifurushi hivyo mpaka hapo hatua zaidi itakapochukuliwa.

Steve kupitia ukurasa wake wa Instagram, alimwomba Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Faustine Ndugulile, kuingilia kati na kutoa japo neno moja kuhusu changamoto iliyokuwapo.

"Mhe Waziri nakuomba sema neno moja tu kwenye suala la bando na vifurushi, hili ni janga na msiba wa wanyonge, wanalia kila kona, najua unajua kwani serikali haijawahi kushindwa kitu kwa kusimama na wananchi wao, ipo tija ya haraka sana kukaa kikao na huzi kampuni" aliandika.



# Klopp ashangaa Trent kuachwa England

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ameshangazwa na kitengo cha Gareth kumwacha Trent Alexander Arnold kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England katika michuano ya kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar.

Trent mwenye umri wa miaka 22 amekuwa kwenye kiwango bora kwa misimu iliyopita akiwa kama beki wa kulia machachari sana.

Lakini msimu huu alianza akiwa na maambukizi ya corona, lakini akajitahidi na kurudi kikosi cha kwanza cha Liverpool.

Katika mahojiano na Daily Mail, Klopp alidai kushangazwa sana na kitendo cha kocha huyo wa England kumwacha Trent.

Alisema ni kweli huu ni muda wao kama makocha kufanya uamuzi mgumu sana ambao watu wengi hawaelewi, lakini kumwacha beki bora wa dunia kwa sasa ni maajabu.

"Kila kocha ana utaratibu wake, hilo liko wazi kabisa,"alisema Klopp.

"Lakini kumwacha nje mchezaji kama Trent ni maajabu makubwa, maana ni mmoja wa walinzi bora kabisa duniani kwa sasa."

Uamuzi wa Southgate umekuwa ukihojiwa sana na huenda pia kikosi hicho kikawakosa Jadon Sancho na Jack Grealish endapo Jesse Lingard ataendelea kufanya vyema.

Trent anaweza akakosa kushiriki michuano ya Euro 2020, endapo Kyle Walker, Kieran Trippier na Reece James wataendeleza makali yao.

Itakumbukwa kuwa Trent amekuwa akijulikana kwa aina ya uchezaji wa beki wa kupanda juu na kushuka pamoja na kusaidia mashambulizi.





# MANE NDIO MCHEZAJI BORA AFRIKA – RASHFORD

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Marcus Rashford, amemtaja mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane kuwa ndiye mchezaji wa Afrika bora zaidi aliyewahi kukabiliana naye kwenye Ligi Kuu England.

Katika kipindi cha maswali na majibu kupitia tovuti ya Twitter, Rashford aliulizwa amtaje mchezaji bora zaidi wa Afrika aliyewahi kukabiliana naye kwenye ligi tangu alipoanza kucheza mwaka 2015.

Na yeye akamtaja Mane kuwa ndio mchezaji bora zaidi kutoka Afrika ambaye amewahi kukabiliana naye.

"Nadhani kuna vipaji vingi vya Afrika kwenye ligi kwa wakati huu, mmoja wao ni Mane," alisema mshambuliaji huyo.

"Nimekabiliana naye mara kadhaa, lakini lazima niseme wazi, yeye ndio mchezaji bora zaidi kutoka Afrika kwa upande wangu mimi."

Rashford amekabiliana na wachezaji mahiri kama Mohamed Salah, Yaya Toure, Pierre-Emerick Aubameyang na Riyad Mahrez, lakini Mane ndio amempa nafasi ya juu kabisa.

# *Konate hana furaha Leipzig*

**DORTMUND,** Ujerumani

WAKATI akiwa anahusishwa zaidi na mpango wa kuhamia Liverpool, beki wa kati wa RB Leipzig, Ibrahima Konate, ameripotiwa kuwa hana furaha na nafasi yake ya sasa kwenye klabu aliyopo.

Liverpool wametajwa kumworodhesha nyota huyo kwenye orodha ya vipaumbele vyao kwenye dirisha lijalo la uhamisho, licha ya mkurugenzi wa michezo wa Leipzig, Markus Krosche kukanusha habari za mpango wa mchezaji huyo kwenda Anfield.

Kwa mujibu wa Sky Deutschland, Konate haridhishwi kabisa na hali yake ya mchezo pale kwenye dimba la Red Bull Arena, baada ya kupigwa benchi katika idadi kubwa ya mechi na Kocha Mkuu, Julian Nagelsmann msimu huu.

Nyota huyo hakuwapo kwa mwezi mzima wa Januari kwa sababu ya jeraha la enka, lakini ametajwa kwenye kikosi kwenye mechi saba zilizopita za Bundesliga.

Licha ya kutajwa kwenye mechi hizo zilizopita, beki huyu amepata nafasi ya kushiriki kwenye mechi tatu tu, ambapo pia hajapata nafasi ya kucheza kwa dakika zote 90 kwa wakati huo.

Kutokuwa na furaha kikosini hapo kunamfanya ahitaji kutafuta changamoto mahali pengine. Ukiachana na Liverpool, Manchester United na Arsenal pia wametajwa kuwania kumsajili wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Konate ni mmoja wa mabeki bora zaidi kwa sasa barani Ulaya.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA AFUNGUKA JUU YA HAALAND, KANE

**Kocha huyo asema kutetereka kiuchumi kunaifanya City ijiweke pembeni katika mbio za...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema klabu hiyo haina uwezo wa kuwasajili washambuliaji, Erling Haaland au Harry Kane licha ya kuthibitisha ataachana na straika wake, Sergio Aguero mwishoni mwa msimu huu.

**Guardiola amesema itakuwa vigumu kupata mbadala wa Aguero ambaye ni mfungaji bora wa muda wote katika klabu hiyo aliyekosa nusu ya msimu kutokana na majeraha.**

Uchumi wa klabu mbalimbali umetetereka katika kipindi hichi kutokana na mlipuko wa corona na hilo halina tofauti kwa upande wa kikosi cha Guardiola.

"Nataka kuwa wazi, labda tutatafuta mchezaji mpya wa kuchukua nafasi ya (Aguero) kwa maana ya (mabao)," alisema Klopp akiiambia BBC Sport.

"Kwa bei hizi, haiwezekani - hatuwezi kumudu. Hiyo haiwezi kutokea. Klabu zote zinapambana kiuchumi na kwetu pia sio tofauti.

"Kwa sasa hali ilivyo inakuwa ngumu sana kwa timu katika dirisha la usajili, hivyo uwezekano wa kuwapata Haaland na Kane ni mdogo mno."

Haaland amekuwa nyota ambaye atazungumza sana kulekea kwenye usajiili wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Klabu kama Manchester United, Barcelona, Real Madrid na PSG zimekuwa zikihusishwa sana na usajili wake.

Kane kwa upande wake anaonekana maisha yamemshinda kule Tottenham Hotspur akiwa anataka kutafuta changamoto mpya, hivyo naye amekuwa akihusishwa kuwaniwa na City.

## ZISIKUPITE

### SALAH NJIA MOJA

LIVERPOOL ipo kwenye wakati mgumu wa kumshawishi mshambuliaji wake, Mohamed Salah, 28, raia wa Misri, kubaki kwenye kikosi hicho, wakati yeye akitaka kutafuta changamoto mpya. ***(ESPN)***

### UNITED, CHELSEA VITANI

MANCHESTER United na Chelsea zote zinawania kumsajili winga wa Real Madrid, Lucas Vazquez, 29. ***(ABC)***

### CHELSEA WAMTAKA AGUERO

CHELSEA inaangalia uwezekano wa kumsajili straika wa Argentina, Sergio Aguero, 32, wakati atakapoondoka Manchester City kipindi cha majira ya joto kinachokuja, kama hawataweza kumsajili Erling Haaland (20), kutoka Borussia Dortmund. ***(ESPN)***

### ODEGAARD KUUZWA

REAL Madrid ipo tayari kumuuza kiungo wake, Martin Odegaard ili kupata fedha za kumnunua Erling Haaland, 22. Odegaard kwa sasa anacheza kwa mkopo katika kikosi cha Arsenal na washikabunduki hao wanataka kumsajili moja kwa moja nyota huyo. ***(Times)***

### MARTINEZ ANUKIA BARCA

BARCELONA inamwangalia fowadi wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez, 23, kama mbadala iwapo watashindwa kumsajili, Erling Haaland. ***(Sport)***

### PSG KUMWACHIA MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain inaweza kufikiria kumuachia kuondoka straika wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, kipindi cha majira ya joto kama mazungumzo ya kuongeza mkataba yatakwama. ***(Le Parisien)***

### WIJNALDUM ATOSWA

BARCELONA inaweza kusitisha mpango wa kumsajili kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum, 30, na badala yake kumfanya Ilaix Moriba mwenye miaka 18 kuwa ndio nguzo muhimu katika msimu ujao. ***(Metro)***

### IHEANACHO KIMEELEWEKA

FOWADI wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 24, anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Leicester kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### KEAN KUREJEA JUVE

JUVENTUS inapanga kumrudisha fowadi wa Everton na Italia, Moise Kean, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Paris St-Germain. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alijiunga na Toffees hao akitokea Juve mwaka 2019. ***(Tuttosport)***

### KANE AIKUBALI SPURS

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho anaamini straika wa England, Harry Kane, 27, ana furaha na hali ilivyo klabuni hapo licha ya kuhusishwa na mpango wa kutaka kuondoka. ***(Standard)***

## Baraza kurejesha heshima Kagera

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza amesema amejipanga kuiongoza vyema timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na kuinusuru isishuke daraja.

Baraza, kocha wa zamani wa Biashara United kibarua chake cha kwanza kitakuwa Aprili 9, mwaka huu ambapo Kagera Sugar itaikaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema kwa muda mfupi aliokaa na kikosi hicho, ameona wachezaji wake wana mabadiliko makubwa tofauti na alivyowakuta.

"Nashukuru kwa kipindi kifupi nilichokaa na wachezaji wangu nimefanya mabadiliko makubwa ambayo nina amini yatatusaidia kufanya vizuri ugenini," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema michezo miwili ya kirafiki ambayo wamecheza dhidi ya timu yao ya vijana imewasaidia kuwajenga na kuwaweka tayari kwa mapambano.

"Mechi za kirafiki tulizocheza zimenisaidia kuwajua zaidi wachezaji pamoja na kugundua upungufu wa kila mmoja wao, ninaahidi kuiweka kwenye nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Baraza.

Aliongeza ana wachezaji wawili ambao ni majeruhi, lakini amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kuwa nyota hao watarejea mapema kikosini.

## Ligi Kuu Zanzibar kurejea J'tano

**Na Hawa Abdallah**

LIGI Kuu Zanzibar inatarajia kuendelea tena kuanzia Aprili 7, mwaka huu baada ya kumalizika kwa kipindi hiki cha maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL), Sheha Mohamed alisema ligi hiyo itaendelea kwa kuanza kuchezwa mechi za viporo vya mzunguko wa tano.

Sheha alisema jumla ya mizunguko saba itachezwa katika hatua ya lala salama huku mizunguko mingine minne itakayobakia itachezwa baada ya kumalizika kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema uamuzi wa kucheza hivyo ulifikiwa katika kikao kilichowakutanisha viongozi wa bodi na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kilichofanyika jana kwa makubaliano ya pamoja.

Kuhusu Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja alisema ligi hiyo itaendelea kuanzia Aprili 8 mpaka Aprili 11, mwaka huu na baada ya hapo pia itasimama kupisha ibada ya funga ambayo itaanza hivi karibuni.

# NAMUNGO FC, NKANA MAJARIBUNI AFRIKA LEO

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC wanatarajia kuwakaribisha Nkana kutoka Zambia katika mchezo wa raundi ya tatu Kundi D utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Pyramids ya Misri ndio inayoongoza katika Kundi D ikiwa na pointi sita sawa na Raja Casablanca, Namungo ikishika nafasi ya tatu na Nkana FC wanaburuza mkia katika kundi hilo huku wakiwa hawajavuna pointi yoyote.**

Namungo itashuka dimbabi ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi ya pili za hatua hiyo ya makundi kwa kukubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Raja Casablanca, mchezo uliopigwa Morocco na ilikubali kichapo kingine kama hicho kutoka kwa Pyramids walipocheza hapa nyumbani.

Nkana wenyewe wanashuka dimbani wakiwa wamepoteza mechi mbili wakifungwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Pyramids na kuchapwa na Raja Casablanca mabao 2-0.

Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Godfroid Okoko, aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mechi ya leo yameenda vizuri na wachezaji wote wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri ndani ya uwanja wa nyumbani.

"Tumejipanga vizuri, lakini tutamkosa Abdulhalim Humud, ila tuna matumaini mazuri baada ya kupata mchezaji mwingine atakayechukua nafasi hiyo," alisema Okoko.

Naye nahodha wa Namungo FC, Reliants Lusajo, alisema wamejipanga vizuri ingawa wanafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani mkubwa kutokana na timu zote kujiandaa na kurekebisha makosa ya michezo yao iliyopita.

"Mechi hii ni muhimu sana, tutahakikisha tunatapa matokeo mazuri, pia tumeandaliwa vizuri kisaikolojia na tuko tayari kupambana katika mchezo huu," alisema Lusajo

Kwa upande wa Kocha wa Nkana FC, Kelvin Kaindu alisema licha ya changamoto ndogo ndogo walizokutana nazo, wamejipanga vizuri kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo wa ugenini.

"Msimu uliopita tulipoteza mechi dhidi ya Simba, ila sasa tumekuja kucheza na Namungo, tunatarajia itakuwa mechi ya ushindani kwa sababu wote tunahitaji kupata mtokeo katika mchezo huo," alisema Kaindu.

Namungo inashiriki mashindano hayo baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kombe la FA msimu uliopita.



Golikipa chaguo la tatu wa Yanga, Ramadhani Kabwili (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa timu hiyo, katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa Aprili 10, mwaka huu jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Nyota watatu wasubiriwa Yanga*

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI watatu wa kimataifa wa Yanga bado hawajarejea nchini kuungana na wenzao kwa ajili ya maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC itakayochezwa Aprili 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi aliwataja wachezaji hao ambao hawajafika ni Haruna Niyonzima aliyekuwa na kikosi cha Timu ya Taifa ya Rwanda, Mukoko Tonombe (DRC) na Said Ntibazonkiza anayeichezea Burundi.

"Nina imani wachezaji wa kigeni ambao bado hawajafika, watarejea ndani ya siku mbili hizi, ninatarajia kuona kikosi kimekamilika ili waendelea na majukumu yaliyoko katika timu yetu," alisema Mwambusi.

Kocha huyo alisema anaamini kikosi chake kitakapokuwa kimekamilika, lengo la kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa msimu huu likiwa chini yake litatimia.

Alisema hana hofu na viwango vya wachezaji hao kwa sababu walipokuwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa waliendelea kujiimarisha na sasa watarejea Yanga wakiwa na mbinu za ziada za kusaka ushindi.

"Wachezaji hao wakifika moja kwa moja wataingia kambini kwa lengo la kuendeleza mapambano ambayo yataipa mafanikio timu yetu," Mwambusi alisema.

Aliongeza kila idara ameipa maelekezo na kubwa amesisitiza umakini na utulivu kwenye safu ya ushambuliaji ambayo mabao yao huipa timu ushindi.

# Michezo

Jumapili Aprili 4, 2021

Nipashe




**Guardiola afunguka juu ya Haaland, Kane** UKURASA 22



Kiungo wa Simba, Mzambia Clatous Chama (kushoto), akifunga bao katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita kutoka DRC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 4-1. **PICHA: SSC**

## Mwakalebela: Yanga kuamua hatima yangu

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, amesema uamuzi wa kukata au kutokata rufaa juu ya adhabu aliyopewa na Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), utafanywa na klabu hiyo inayoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Mwakalebela aliliambia gazeti hili jana uamuzi huo umemuumiza kwa sababu anaamini alikuwa akitekeleza majukumu yake ya kulinda maslahi ya Yanga.

"Nimeiachia klabu iamue, ila nimepokea hukumu hiyo hasi, imeniuma," alisema Mwakalebela kwa kifupi.

Kamati ya Maadili ya TFF juzi ilitangaza kumfungia Mwakalebela kifungo cha miaka mitano cha kutojishughulisha na mpira wa miguu pamoja na kumtoza faini ya Sh. milioni tano baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la uchochezi.

Adhabu hiyo ilitolewa kwa kuzingatia kifungu cha 73 (4), cha Kanuni za Maadili za TFF toleo la mwaka 2013. Pia Mwakalebela alikutwa hatiani kwa kosa lingine ya kutoa taarifa za uongo ambalo alilitenda Oktoba Mosi, 2020.

# *Simba yatinga robo fainali kibabe*

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## ●●● Yairarua AS Vita na kuongoza Kundi A, yagawa biriani ya Pasaka na...

PAMOJA na kukosa mabao mengi ya wazi, wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, imetinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo baada ya kuirarua AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mabao 4-1 katika mchezo wa Kundi A uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Kiungo mshambuliaji wa Simba, Luis Miquissone, ameweka rekodi ya kufunga bao kwenye mechi zote tatu ambazo Simba imecheza nyumbani katika hatua hiyo ya makundi.**

Miquissone alifunga bao wakati Simba ikicheza dhidi ya Al Ahly, timu yake ikifunga bao pekee, Februari 23 na goli lingine Machi 16, mwaka huu Simba ikichapa Al Merreikh mabao 3-0 huku rekodi ya Simba pamoja na golikipa, Aishi Manula ya kutoruhusu bao kwenye hatua ya makundi ilifutika jana kwa bao la kufutia machozi la AS Vita.

Simba iliandika bao la kwanza dakika ya 29 kupitia kwa Miquissone aliyepiga shuti kali baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Morrison aliyewalamba chenga mabeki kadhaa wa AS Vita, kabla ya kumpasia mfungaji.

Dakika mbili badaye, AS Vita walisawazisha bao kupitia kwa Zemanga Soze aliyemchungulia Manula na kupiga shuti la pembeni, lililogonga nguzo kabla ya kujaa wavuni.

Wakati kila mmoja akiamini mechi hiyo itakwenda mapumziko kwa sare, Clatous Chama aliukwamisha mpira ndani ya wavu, baada ya krosi ya Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' kuleta kizaazaa golini, kabla ya mfungaji kuukwamisha wavuni na kuwaacha mabeki wa AS Vita na kipa wao, Simon Omossola wakishangaa.

Kipindi cha pili Simba ilibadilisha mfumo wake kwa kukaa nyuma ya mpira na kushambulia kwa kushtukiza, huku AS Vita ikijilipua kwa kutaka ushindi wa lazima, na hiyo iliwagharimu, kwani wapinzani wao walitumia kushambulia kwa kushtukiza ambapo walikuwa hatari zaidi.

Hii ni baada ya kuwatoa Chris Mugalu aliyekosa mabao yapatayo matano ya wazi na nafasi yake kuchukuliwa na Meddie Kagere, Morrison naye akitoka na nafasi yake kuingia, Rally Bwalya ambaye alikuwa kivutio na tishio kwa ngome ya AS Vita.

Ni Bwalya aliyeanza kuihakikishia Simba kunusa hatua ya robo fainali baada ya kufunga bao la tatu kwa shuti kali akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, alipopata pasi kutoka kwa Mzambia mwenzake, Chama.

Alikuwa ni Chama tena dakika sita kabla ya mechi kumalizika, akifunga bao la nne, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Miquissone.

Kwa matokeo hayo, Simba imeweka rekodi na kurudia kile ilichokifanya Machi 16, 2019, ilipotinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa kuifunga timu hiyo hiyo ya AS Vita mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa zamani Uwanja wa Taifa.

Kwa matokeo hayo, Simba bado inaongoza Kundi A ikiwa na pointi 13 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote, hivyo kuwa kinara wa kundi hilo hata ikipoteza mechi yake ya mwisho itakayochezwa Aprili 9, mwaka huu dhidi ya Al Ahly nchini Misri.

Ni baada ya Al Ahly kutoka sare ya mabao 2-2 nchini Sudan dhidi ya wenyeji Al Merreikh na kufikisha pointi nane katika mchezo wa jana jiji Khartoum nchini Sudan. Simba na Al Ahly ndizo zilizofuzu kwenye Kundi A, huku AS Vita iliyosalia na pointi nne na Al Merrikh pointi mbili zikishindwa kusonga mbele.

Wageni AS Vita walitangulia kuingia uwanjani, walifika kwenye uwanja huo saa 8:07 mchana kwa kutumia basi la Azam FC baada ya kugomea lile waliloandaliwa na wenyeji wao kwa kuogopa hujuma.

Simba iliwaandalia AS Vita basi la Kampuni ya Happy Nation na badala yake Wakongomani hao walipanda basi la Azam lenye namba za usajili T 420 CSN.

Wakati Simba waliingia uwanjani saa 8:27 kwa basi lao la zamani licha ya kuwapo kwa taarifa kwamba uongozi umeunua basi lingine jipya ambalo lilionekana juzi likiendelea kubandikwa nembo mbalimbali za klabu hiyo.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, ndiye alikuwa mtu wa kwanza kushuka katika basi akifuatiwa na mshambuliaji, Chris Mugalu wakati nahodha wa timu hiyo, John Bocco hakuwa miongoni mwao na baadala yake alifika uwanjani hapo na usafiri binafsi.

Katika hatua nyingine, mashabiki wa timu hiyo walijitokeza kushuhudia mtanange huo walioonekana kufuata maelekezo yaliyotolewa na mamlaka husika kuhusiana na kujikinga na ugonjwa wa corona kama walivyotakiwa.

Mbali na mashabiki waliokuwa ndani, pia nje ya uwanja mashabiki wengine walijitokeza kuangalia mchezo huo kupitia vibanda umiza.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >